# KUCHUNGUZA DHAMIRA KATIKA HADITHI ZA WATOTO: MFANO KUTOKA WILAYA YA TEMEKE

**WINIFRIDA MATASO WARIOBA**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UMAHIRI YA KISWAHILI (M.A. KISWAHILI) KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2023**

## UTHIBITISHO

Aliyeiweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasinifu hii iitwayo **Kuchunguza Dhamira katika Hadithi za Watoto: Mfano kutoka Wilaya ya Temeke** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya shahada ya Uzamili katika Kiswahili (M.A Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**……………………………………..**

Dkt. Mohamed Omary Maguo

**(Msimamizi)**

**Tarehe** …………………………….

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili sehemu yoyote ile ya tasinifu hii, kwa njia yoyote kama vile kielektroniki, kurudufu nakala au kurekodi bila ya idhini ya mwandishi wake au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

## TAMKO

Mimi, **WINIFRIDA MATASO WARIOBA,** ninakiri kuwa tasinifu hii inayohusu ‘Kuchunguza Dhamira katika Hadithi za Watoto: Mfano kutoka Wilaya ya Temeke, ni kazi yangu mwenyewe. Haijatolewa na haitatolewa kwa mahitaji ya kutunukiwa shahada ya Uzamili au shahada nyingine yoyote katika Chuo Kikuu kingine chochote.

**Saini……………..……………….**

**Tarehe …………………………**

# TABARUKU

Kwa heshima na taadhima naitabaruku kazi hii kwa marehemu Mama yangu kipenzi Bi, Prisca Magoli Kiyongo, nakushukuru sana mama yangu kipenzi kwa kunizaa, kunisomesha na hata kunilipia ada nianze masomo ya shahada ya uzamili lakini kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu uliaga dunia, hongera sana mama yangu kwa kazi kubwa uliyoifanya laiti kama ungelikuepo ungeliona matunda ya mbegu uliyoipanda. Baba yangu Bw, Seilasie Mataso Warioba nakushukuru kwa malezi na kunipa misingi mizuri ya maisha nisome sana maana elimu haina mwisho kwa mapenzi ya mwenyezi Mungu uliaga dunia January 29 mwaka huu 2023, Mungu akurehemu.

Pia naitabaruku kazi hii kwa wanangu vipenzi; Prince Samwel Godfrey, Precious Hollie, Mato/Kadada, Baby Tv, Leroy na Prince Looqman kwa kunivumilia muda wote wa masomo mpaka utafiti.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu, muumba mbingu na dunia na vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana. Ambaye amenijaalia afya njema na kuniwezesha kufikia kiwango hiki cha elimu na uwezo wa kuifanikisha kazi hii. Kufanikiwa kwa kazi hii kumetokana na msaada wa hali na mali kutoka kwa watu na asasi mbalimbali, si rahisi kuwataja wote lakini nitawataja baadhi yao kwa niaba ya wengine waliochangia kwa namna moja au nyingine.

Pili, natoa shukrani zangu za dhati kwa msimamizi wangu, Daktari Mohamed Omary Maguo ambaye mawazo, fikra na mwongozo wake ndiyo uliyonisaidia na kunipa msukumo wa kufanya kazi hii mpaka kufikia kiwango hiki. Pia nashukuru uongozi wa Wilaya ya Temeke kupitia kata ya Kijichi, Mtoni, Chamazi, Mbagala kuu na Temeke kwa kunipokea vyema na kunipa kibali cha kufanya utafiti huu.

Tatu, nawashukuru maprofesa na wahadhiri wote wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Walionifundisha kozi ya shahada ya Uzamili (Fasihi). Kwa msaada wao wa kitaaluma, maelekezo na ushauri kwa muda wote wa darasani. Mawazo yao yalinisaidia na kuniongoza mpaka kufikia hapa nilipo. Vilevile, nawashukuru sana wanafunzi wenzangu wa shahada ya uzamili mwaka 2019-2021, hasa wale wa Fasihi ya Kiswahili tawi la Zanzibar na Dar es salaam, kwa kunipa michango ya mawazo ambayo yamenisaidia kuandaa pendekezo la utafiti lililonifikisha kwenye hatua ya kufanikisha kuandika tasinifu hii.

Nne, natoa shukrani zangu za dhati kwa familia yangu, kwa kunisimamia, kunisaidia na kunivumilia hapa na pale mpaka kuifanikisha kozi hii. Nawashukuru watu wangu

wa nguvu na muhimu kama, Godfrey Lubango, Edina Warioba, Anna Warioba, Omar Bakary, Patric Thomas Fulla Mungu awabariki wote.

## IKISIRI

Tasinifu hii ilihusu "**Kuchunguza Dhamira katika Hadithi za Watoto: Mfano kutoka Wilaya ya Temeke."** Utafiti huu uliongozwa na lengo kuu na malengo mahsusi mawili, lengo kuu lilikuwa ni kuchunguza dhamira katika Hadithi za Watoto katika Wilaya ya Temeke na na malengo mahususi la kwanza ni Kuchambua dhamira katika hadithi za Watoto katika Wilaya ya Temeke na lengo la pili ni kubainisha ujumbe unaopatikana katika hadithi za Watoto katika Wilaya ya Temeke. Data za msingi za utafiti huu zilikusanywa kwa mbinu ya ushuhudiaji, dodoso na uchambuzi wa kinyaraka. Mjadala na uchambuzi wa data zilizowasilisha uliongozwa na nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa dhamira mbali mbali zilizoibuka kutokana na utafiti na uchambuzi uliofanywa. Dhamira hizo ni usafi wa mazingira, wizi katika jamii, ujasiriamali, mmonyoko wa maadili, ulevi katika jamii, uvivu na uzembe katika jamii na umoja na mshikamano. Ujumbe uliojitokeza katika hadithi za watoto ni pamoja na usafi wa mazingira ni jambo la muhimu katika jamii zetu ivo kila mtu ayapende mazingira yake, wizi ni tamaa na yaweza kumfikisha mtu pahala pabaya, majivuno siyo jambo zuri katika maisha, kiburi na dharau sio kitu kizuri katika maisha, umoja na mshikamano ni jambo la msingi mno Wananchi waishi kwa kushirikiana, ulevi ni adui wa maendeleo na ujumbe mwingine ni kila mtu anapaswa kujitegemea katika maisha na kufanya kazi kwa bidi. Utafiti huu umetoa mapendekezo kwa watafiti wengine na jamii kwa ujumla, wazidi kufanya tafiti zaidi kuhusu hadithi za watoto katika wilaya mbalimbali ili waweze kuzibainisha dhamira na mafunzo katika hadithi za Watoto, na kuvifanya vizazi vijavyo viweze kufaidika na hadithi hizo.

## YALIYOMO

UTHIBITISHO ........................................................................................... ii

HAKIMILIKI............................................................................................... iii

TAMKO.. .................................................................................................... iv

SHUKRANI ................................................................................................ vi

IKISIRI.. ..................................................................................................... viii

YALIYOMO ................................................................................................ ix

ORODHA YA MAJEDWALI ........................................................................ xiii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA JUMLA ........................................... 1**

1.0 Utangulizi ........................................................................................ 1

1.1 Usuli wa Tatizo La Utafiti ........................................................................ 1

1.2 Tatizo la Utafiti ...................................................................................... 7

1.3 Malengo ya Utafiti .................................................................................. 8

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti ............................................................................. 8

1.3.2 Malengo Mahsusi ................................................................................. 8

1.4 Maswali ya utafiti ................................................................................... 8

1.5 Umuhimu wa Utafiti ............................................................................... 8

1.6 Mipaka ya Utafiti .................................................................................... 9

1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake ....................................................... 10

1.8 Mpangilio wa Tasnifu ............................................................................. 10

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ......................................................................... 12**

2.1 Utangulizi ........................................................................................ 12

2.2 Dhana ya Hadithi ............ 12
2.2.1 Dhana ya Fasihi ya Watoto ............ 13
2.2.2 Dhana ya Fasihi Simulizi ............ 15
2.3 Maana ya Dhamira ............ 15
2.4 Mapitio mbalimbali kuhusu Hadithi ............ 16
2.5 Pengo la Utafiti ............ 21
2.6 Mkabala wa Kinadharia ............ 21
2.6.1 Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ............ 22
2.7 Hitimisho ............ 25

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ............ 26**

3.1 Utangulizi ............ 26
3.2 Eneo la Utafiti ............ 26
3.3 Usanifu wa Utafiti ............ 27
3.4 Vyanzo vya Data ............ 27
3.5 Kundi Lengwa ............ 27
3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ............ 29
3.6.1 Ushuhudiaji wa Utambaji Hadithi ............ 29
3.6.2 Dodoso ............ 30
3.6.3 Upitiaji wa Kinyaraka ............ 30
3.7 Uchambuzi wa Data ............ 30
3.7.1 Mbinu ya Kimaelezo ............ 31
3.7.2 Mkabala wa Kidhamira ............ 31
3.8 Kuaminika na Ubora wa Data ............ 32

3.9 Itikeli ya Utafiti .......... 32
3.10 Hitimisho .......... 34

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI .......... 35**

4.1 Utangulizi .......... 35
4.2 Maana ya Dhamira na ujumbe katika kazi ya Fasihi .......... 35
4.2.1 Usafi wa Mazingira .......... 36
4.2.2 Wizi .......... 39
4.2.3 Ujasiriamali .......... 41
4.2.4 Mmomonyoko wa Maadili .......... 43
4.2.5 Umoja na Mshikamano .......... 44
4.2.6 Ulevi .......... 45
4.2.7 Uvivu na Uzembe katika Jamii .......... 47
4.3 Hitimisho .......... 49

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .......... 50**

5.1 Utangulizi .......... 50
5.2 Muhutasari wa Utafiti .......... 50
5.3 Utoshelevu wa Nadharia .......... 51
5.4 Matokeo ya Utafiti .......... 51
5.4.1 Lengo la Kwanza .......... 51
5.4.2 Lengo la Pili .......... 52
5.5 Mapendekezo .......... 52
5.5.1 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine .......... 52

5.5.2 Mapendekezo kwa Wanajamii ........................................................................ 52

5.6 Hitimisho.......................................................................................................... 53

**MAREJELEO………… ......................................................................................... 54**

**VIAMBATISHO……… ......................................................................................... 60**

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 3.1 Jedwali la watafitiwa........................................................................ 28

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.0 Utangulizi

Utafiti huu umechunguza kuhusu "Dhamira katika Hadithi za Watoto: Mfano kutoka Wilaya ya Temeke". Mada hii imeteuliwa ili kuziba pengo la kiutafiti lililodhihirika baada ya kudurusu kazi tangulizi mbali mbali. Sehemu hii inashughulikia vipengele muhimu ambavyo ni usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake, mpangilio wa tasinifu na hitimisho.

## 1.1 Usuli wa Tatizo La Utafiti

Bila shaka umepata kushuhudia watu wakiimba nyimbo au kughani mashairi kwenye sherehe au tukio la kijamii, au kama umeishi kijijini umeona au umeshiriki katika kazi za ushirikiano hukosi kuona watu wakiimba, kusogoa, kutamba, kutaniana hata kucheza ngoma wakati wakiendelea na kazi. Umepata kumuona mzee akimuasa kijana kwa kumtamkia methali au kumuhadithia hadithi yenye funzo fulani? Matukio yote hayo ni mifano ya dhima au utendakazi wa fasihi (Mulokozi 2017). Wakazi wa Wilaya ya Temeke hutumia fasihi ya hadithi katika maisha yao ya kila siku kama sehemu ya kuendeleza utamaduni wao uliozoeleka toka kizazi hadi kizazi kwa ajili ya kuelimisha, kuburudisha, kufundisha na kukemea maovu. (Maelezo ya mtafitiwa mzee maarufu kata ya Kijichi Kurunge Said. 20/7/2021)

Fasihi Simulizi ni fasihi ambayo imekuwa na umuhimu mkubwa sana kwenye jamii ikiwemo kuelimisha, kuburudisha, kukemea maovu na kufanya jamii iachane na mienendo isiyofaa katika jamii kwa mfano ukeketaji, mauaji ya vikongwe kupitia

fasihi ya nyimbo au ngonjera jamii huelimika (Mulokozi 2007). Historia inaeleza kuwa baada ya binadamu kuanza kuishi pamoja, ilizuka haja ya mawasiliano ambayo yaliibua fasihi na ndio jamii iliitumia katika kuielekeza jamii vipengele vya maisha. TAKILUKI (1982) wanasema kila jamii ina fasihi yake ambayo inawasaidia kuwarahisishia mawasiliano.

Kwa mujibu wa https:/sw.wikipedia.org anasema; hadithi ni tungo za fasihi simulizi zitumiazo lugha ya nadharia kuelezea mambo mbalimbali katika jamii. Hadithi ni utungo ulioenea sana duniani. Mataifa mengi duniani hutumia sanaa hii ili kuelimisha na kuburudisha baada ya kazi mbalimbali katika jamii zao. Mfano nchi za kiarabu hutumia sanaa hii kuasa na kuelimisha mambo mbalimbali kuhusu misingi ya imani ya Uislamu, mfano kupitia hadithi za Mtume Muhammad Swalallahu Alayh Wasallam, hadithi za “Alfu Lela U Lela” ambayo ni tafsiri ya kwanza ya kiarabu ilichapwa Misri miaka ya 1830.

Kihistoria wahakiki Edgar Allan, Paul Blander Matthews ndio wanahusishwa kuanzisha kwa utanzu wa hadithi fupi. Wamitila (2002: 66) katika fasihi andishi katika maisha ya Magharibi. Edgar ndiye aliyelitumia neno la kiingereza la “short story”kwa mara ya kwanza (Henry, 1995). Baadae utanzu huu wa hadithi ulienea na kuingizwa katika fasihi andishi za lugha nyinginezo Ulaya.

China nayo haikuwa nyuma ina hadithi nyingi mno na maarufu mfano “Hadithi za Mashetani”, haya ni maandishi makubwa katika historia ya fasihi ya Kichina katika miaka mia mbili iliyopita hadithi hiyo imetafsiriwa kwa lugha zaidi ya ishirini.

Hivyo huo ni muendelezo mzuri wa utanzu wa hadithi duniani. [http://www.yoair. com]/sw/blog/lgr

Nchi ya China hapo zamani ilikuwa ni maarufu kwa sababu hadithi zake mara nyingi zilizungumzia juu ya mapambano ya watu na mto hatari na juu ya mapambano yao ya ukaidi kwa shirika la uchumi na kilimo. Hadithi za zamani zilielezea jinsi Wachina walivyopambana na mafuriko yaliyosababishwa na mto Njano. Maji ya mafuriko hayo yalileta majanga mabaya na kuharibu vijiji na mazao, hivyo hizi ndio hadithi zilizohadithiwa vizazi hadi vizazi.

Huko Ugiriki kuna mitholojia ya kigiriki, hii ni jumla ya elimu ya visasili au mitholojia ya ugiriki ya kale, yaani ukusanyaji wa masimulizi na hadithi kuhusu vyanzo, miungu na mashujaa wa ugiriki pamoja na sehemu ya dini ya Ugiriki ya kale kulikuwa na masimulizi ya hadithi ambayo yalizungumzia maisha yao kwaa ujumla. [ailyheadlines.com]

Masimulizi ya hadithi Romani, Waroma ni watu wa dola la Roma lililotawala eneo kubwa la Ulaya, Asia ya kaskazini na Asia ya Magharibi watu wa mji wa Roma nao wana fasihi yao , mfano ni hadithi za Kirumi kuna hadithi kuhusu kusafiri maisha na jinsi mji wa Roma ulivyoanzishwa. Habari hizi zote zilikuwa katika masimulizi na baadae ziliwekea katika maandishi. Hadithi hizi zimekuwa zikiendelea mpaka sasa na maelfu ya wageni hujitokeza kutalii, kuzisoma, kutazama vivutio hivyo vizuri vya utalii katika mji wa Italia, mfano ni hadithi ya “Dracula ya Castle katika mji wa Komas. http://sw.atomiyme.com

Masimulizi ya hadithi Afrika, fasihi hii ya Kiafrika inamaanisha maandiko kuhusu na kutoka Afrika , haya ni masimulizi, ganizi (kutokana na kugani au kusimulia) ni fani yenye kusimulia habari fulani ndiyo sifa kuu ya hadithi, hivyo basi hii ni fasihi ya kimasimulizi na fani zake huwa na sifa za kuelezea matukio katika mpangilio mahsusi, wahusika au watendaji yenye kutumia lugha ya mjazo yenye maudhui ya kweli au ya kubuni. Afrika nchi nyingi zilitumia fasihi kama njia ya kuelimisha, kuburudisha, kufundisha na kukemea maovu kwa kupiitia ushairi, semi, maigizo na hadithi (Mulokozi 2017).

Jamii za watu kutoka Afrika zilitumia hadithi kama nyenzo ya kufundishia vijana na watoto maadili mema kupitia masimulizi. Ifuatayo ni mifano ya fasihi za Kiafrika; fasihi simulizi ya Afrika ya Magharibi ijumuishayo “Visa vya Sundiata” “Visa vya Dinga” kutoka dola la kale la Ghana. Ngano za Kiafrika kama hadithi za “Ulaghai” kuhusu wanyama wadogo hutumia akili zao kushinda mapambano au kuwahadaa wanyama wakubwa, “Hadithi ya Tambuka” au “Utendi wa Tambuka” (Mulokozi 2017).

Baada ya nchi za Afrika kupitia katika nyakati za ukoloni kazi nyingi za kifasihi maudhui yalihusu ukoloni na namna ya kujikomboa hivyo hata hadithi zilizosimuliwa wakati huo maudhui makuu yalihusu ukoloni. Mfano hadithi ya “Kibanga Kampiga Mkoloni”. Hadithi hii ni kutoka masimulizi ya kabila la Waikizu kutoka mkoa wa Mara.

Baada ya ukoloni ukombozi uliongezeka na kupelekea kusoma na kuandika hivyo hata hadithi zilianza kuandikwa katika vitabu na machapisho madogo na wakati wa

mwanzo zilihadithiwa tu. Mfano wa waandishi hao ni kama; Wole Soyinka, Shaaban Robert, Chinua Achebe, Ayi Kwei Amah, Mariam Ba, Sembene Ousmene, Ngugi wa Thiongo na wengine wengi. (Mwalimuwakiswahili.co.tz//.nov18. 2018)

Hadithi za watoto ni masimulizi/ganizi au fani yenye kusimulia habari fulani kuhusu watoto au wanyama na huwa ni usimulizi wenye mpangilio wa matukio, wahusika wachache yaani wanyama na binadamu, lugha rahisi yenye mchanganyiko wa nyimbo na huwa na maudhui ya kweli au kubuni na lengo kuu huwa ni kutoa funzo au elimu kwa watoto na kuburudisha (Henry 1995).

Mada inayohusu hadithi za watoto imejadiliwa katika kazi nyingi na watafiti mbalimbali. Miongoni mwa watafiti hao ni kama wafuatao;- Ali (1995) alifanya utafiti wake katika kutathmini uhusika wa mwanamke katika hadithi simulizi za wapemba. Mbarouk (2015) nae alifanya kuhusu Athari za sayansi na teknolojia katika hadithi za watoto katika wilaya ya Micheweni Pemba. Naye Mzee (2015) kuchambua maudhui yanayopatikana katika hadithi za watoto katika jamii ya wapemba. Utanzu huu wa hadithi umekuwa na umuhimu mkubwa sana katika jamii, mfano kitanzu cha hadithi za watoto matendo, utumizi wa wahusika wanyama na binadamu na maelezo yatolewayo moja kwa moja huwa ni funzo tosha ambalo hutumika kutoa somo kwa watoto na kwa wakubwa pia katika jamii yoyote ile. Kwa mfano hadithi za watoto hutumia wanyama kama fisi huwasilisha tamaa na kutoridhika, sungura huwakilisha ujuzi na ujanja.

Hamad (1981) anasema hadithi za watoto huwa fupifupi, hutumia muundo wamoja kwa moja ili zieleweke kwa urahisi ingawa ni fupi fupi lakini ujumbe hufikishwa

ipasavyo na lengo la kufanya hivyo ni kuendana na kasi ya walengwa wa hadithi hizo ambazo ni watoto kwa maana akili zao hazijakomaa au kupevuka ipasavyo kuwapa vitu vingi vya kusoma na kusikiliza na kama ukilazimisha basi unaweza kufanya wasielewe na wachoke kusikiliza hadithi unayo simulia au kusomwa. Hadithi huanza na mianzo maalum na miisho maalum yani huanza kwa kusema;

*"Paukwa… Pakawa!*

*"Hadithi … Hadithi ... Njooo"*

Huisha kwa miisho maalumu kama vile, hadithi yangu imeishia hapo! au wakaishi kwa raha mustarehe hii ni kwa mujibu wa (www.gafkosft.com) Utambaji wa hadithi za watoto hutumia nyimbo, hizi husaidia kufikisha ujumbe kwa urahisi zaidi, pia nyimbo hutumika kwa ajili ya kuburudisha wasikilizaji au wasomaji wa hadithi hizo. Hakuna uthibitisho ambao unaonyesha tarehe na mwezi maalum ambapo sanaa na fani ya hadithi ilianza bali huonyesha kuwa ilianza mwanadamu alipo jitambua nakupata urazini ndipo akaanza kuitumia fasihi kama sanaa ya hadithi wazee na watoto walikutana nyakati za jioni baada ya mihangaiko na kazi mbalimbali wakaanza kutambiana hadithi na hadithi hizi zilitumika kuonya, kuelimisha, kushauri, kustarehesha na kuburudisha (Mulokozi, 2017).

Ndungo na wenzake (1991), utanzu wa hadithi ulikuwa na madhumuni ya kusimulia hadithi au kutamba hadithi, lengo mahsusi la kusimulia hadithi ni kuburudisha au kutumbuiza wasikilizaji na utanzu huu ulipitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya mdomo. Mbali ya watafiti hao lakini hakuna mtafiti ambae amejikita katika kutafiti dhamira zinazoibuka katika hadithi za watoto katika Wilaya ya Temeke na ndicho kilichomsukuma mtafiti afanye utafiti huu.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Mada ya utafiti huu ni kuchunguza dhamira katika hadithi za Watoto: Mfano kutoka Wilaya ya Temeke wandishi wachache ambao wameandika kuhusu hadithi za watoto, mfano Omary (2013), Haji na wenzake (2007) na wengine lakini hawakufanyia utafiti kwa dhamira za hadithi za watoto katika Wilaya ya Temeke.

Tatizo la utafiti huu limetokea mara baada ya kudurufu kazi tangulizi na mapitio mbalimbali ya kazi za utafiti ambayo yameelezea kuhusu hadithi kuna watafiti mbalimbali walioelezea suala la hadithi lakini mtafiti kwa uchunguzaji mzuri hajona mtafiti mwingine aliyeongelea suala kuhusu hadithi za watoto: mfano kutoka wilaya ya Temeke hivyo hili likamsukuma mtafitikufanya utafiti huu na alipata ushirikiano mzuri.

Pia vijana wengi huyakosa maadili yatokanayo na fasihi simulizi zinazofundishwa katika jamii zao hasa wakati wa masimulizi ya hadithi ndio maana siku hizi vijana wa shule za sekondari, msingi  na vyuo kukitokea jambo kidogo wakakwazika badala ya kusubiria ufafanuzi wa jambo hilo kutoka kwa wakuu wao vijana hao huanza kufanya fujo na migomo isiyokua na tija wala  maana ambayo huiletea jamii hasara na athari kubwa. Mfano siku hizi kuna wimbi la vijana kuchochewa na kupewa pesa na wanasiasa ili wafanye fujo katika jamii hili ni jambo baya na hatari sana kwa maisha ya wanajamii kwa sababu wengine huumia na kupoteza uhai.

Hivyo basi utafiti huu uliofanyika umesaidia vyema kukumbusha wazazi na walezi wawe wasimaizi wazuri wa watoto na vijana katika jamii kwa kuwafundisha maadili mema yatokanayo na hadithi ikiwemo tabia njema, uadilifu, uvumilivu na uzalendo

nchini mwao kwa kuwasimulia hadithi na kuwaimbia nyimbo na magani yenye kufundisha uzalendo ili waje kuwa raia wanaoipenda nchi yao.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahususi mawili.

### 1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhamira katika hadithi za watoto katika Wilaya ya Temeke.

### 1.3.2 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya utafiti huu ni:

i) Kuchambua dhamira zinazopatikana katika hadithi za watoto katika Wilaya ya Temeke.

ii) Kubainisha ujumbe unaopatikana katika hadithi za Watoto katika Wilaya ya Temeke.

## 1.4 Maswali ya utafiti

i) Ni dhamira zipi zinazojitokeza katika hadithi za watoto katika Wilaya ya Temeke?

ii) Ni ujumbe gani unaopatikana katika hadithi za watoto katika Wilaya ya Temeke?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umeonekana kuwa na umuhimu mkubwa kama ifuatavyo:-

Utafiti huu umekuwa na umuhimu katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na eneo la kiuchambuzi ambapo kwa kuchambua dhamira za hadithi za watoto kwa

kiasi kikubwa itatoa faida kubwa kwa wanataaluma na jamii kwa ujumla kujifunza mafuzo mazuri na yenye maadili kutoka katika hadithi mbalimbali zilizosimuliwa na kuhadithiwa. Kwahiyo kupitia utafiti huu utafanyika msingi mzuri kwa wanataaluma kufahamu vyema utanzu huu wa hadithi za watoto na wao kuvutiwa na kufanya tafiti zaidi kwa kuchunguza hadithi za watoto.

Kwa upande wa nadharia, utafiti huu umejenga msingi imara wa kinadharia kwa kufahamu dhamira na uhalisia wake katika jamii hususani kwa kutumia mkabala wa nadharia ya sosholojia ya fasihi ambayo huichambua kazi ya fasihi kwa kuzingatia hali ya jamii inamozaliwa na kukuzwa sanaa hiyo, hivyo kwa uchambuzi makini wa hadithi za watoto tumeibua dhamira nyingi na mbalimbali zenye kuiakisi jamii kwa uhalisia wake.

Kijamii, utafiti huu utakuwa ni chachu na dira kwa kutoa mwanga kwa jamii katika wilaya ya Temeke kwa jumla, kwa kuzifahamu dhamira zinazopatikana ndani yake kutawafanya waziendeleze na kuzishajihisha kwa watoto wazidi kuzitumia katika maisha yao yote ili waikuze na kuhifadhi fasihi simulizi Wilayani Temeke.

### 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umechunguza dhamira  katika hadithi za watoto katika Wilaya ya Temeke. Maeneo yaliyochunguzwa ni kata za Kijichi, Chamazi, Mtoni, Temeke na Mbagala kuu  ukiwa na lengo la kuchunguza dhamira na ujumbe uliojitokeza katika hadithi hizo, na haukujishughulisha na kitu kingine chochote kile. Maeneo hayo yameteuliwa kwa kuwa yana data na taarifa zitazohitajika katika ukamilishaji wa malengo mahsusi yaliyobainishwa. Mjadala na uwasilishaji wa data umeongozwa na nadharia ya Sosholojia ya fasihi.

## 1.7 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Katika kazi hii mtafiti amekutana na vikwazo mbalimbali, vlivyompa ugumu wa matumizi ya mbinu na zana za kukusanyia data. Changamoto hizo ni pamoja na mazoea waliyonayo baadhi ya wakazi wa wilaya ya Temeke, kuona kwamba hadithi za watoto ni kama mchezo tu na kitu kinachowapotezea muda wakikaa kusikiliza na kusimulia hivyo si jambo la muhimu sana kama mtafiti akitaka kusimuliwa hadithi aende huko kwa watoto. Changamoto hii aliitatua kwa kuelimisha jamii na kuwashawishi kuepukana na dhana hiyo potofu kwa kuwaelezea lengo la utafiti na umuhimu wake hivyo walimuelewa na walikubaliana nae wakampa ushirikiano mzuri. Changamoto nyingine ni suala la muda hii ilitokea wakati wa kutembelea maeneo ya shuleni na mtaani, tuliandaa ratiba ya kufika shuleni na mtaani pamoja na uongozi wa eneo husika lakini muda ulipofika wenyeji walisema bado wapo na kazi nyingine kuwa wasingeweza kusailiwa muda huo, changamoto hii ilitatuliwa kwa mtafiti kuwafuata wasailiwa kulingana na fursa yao ya kupatikana hasa nyakati za jioni.

## 1.8 Mpangilio wa Tasnifu

Tasinifu hii imeundwa kwa sura tano ambapo sura ya kwanza inahusu utangulizi. Katika sura hii kumewasilishwa vipengele mbalimbali kama vile usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake na mpangilio wa tasnifu. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia na sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti zikihusisha usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa; data za msingi na data za upili, mbinu za

kukusanyia data; usomaji makini na upitiaji wa nyaraka, mbinu za uchambuzi wa data; mkabala wa kimaelezo, usahihi wa data na maadili ya utafiti. Sura ya nne ni uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti na sura ya tano ni hitimisho, muhtasari na mapendekezo.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mapitio ya machapisho na kazi tangulizi mbali mbali zinazohusiana na mada iliyotafitiwa. Kazi tangulizi ambazo mtafiti amezieleza katika sehemu hii ni zile ambazo zinahusu maana ya hadithi, maana ya fasihi ya watoto, aina ya hadithi, maana ya fasihi simulizi, dhana ya dhamira, tafiti mbalimbali zilizofanywa kutokana mada husika, Ili tuweze kugundua kile ambacho watafiti wengine wamekifanya au wametafiti kutokana na tafiti zao, jambo ambalo limemfanya mtafiti aweze kupata mwendelezo mzuri wa uchunguzi wa dhamira katika hadithi za watoto, ikwemo na mkabala wa kinadharia, kitu ambacho kinamuongoza mtafiti katika utafii huu. Mapitio haya yanahusisha majarida, vitabu, tasinifu na makala za kiutafiti, kiuchambuzi na kiuhakiki. Kwa kawaida, mapitio husaidia kubaini pengo la kiutafiti linalopaswa kushughulikiwa katika uchunguzi unaohusika (Upagade & Shende, 2010). Katika sehemu hii vipengele vinavyohusiana na mada teule vimeelezewa kama ifuatavyo.

## 2.2 Dhana ya Hadithi

Hadithi ni simulizi za kinathari ambazo huwa na wahusika ambao huzungumziwa katika hadithi hiyo. Wahusika katika hadithi za fasihi wanaweza kuwa niwanadamu au viumbe vyovyote vilivyopewa sifa au uwezo wa kibinadamu. Hamad na wenzake (1981). Hadithi katika fasihi simulizi, aghalabu huwa ni fupi fupi, hivyo, hutumia mtindo wa moja kwa moja ili ieleweke kwa urahisi. Katika maelezo hayo ya utambaji wa hadithi fanani pia, ana nafasi ya kufikisha ujumbe kwani hutegemea

namna alivyo na uwezo wa kuelezea kwa kutumia viungo vyake vya mwili mbali na kutumia maelezo. Aidha, hadithi hutumia mbinu ya nyimbo. Mbinu hii husaidia kufikisha ujumbe kwa hadhira na kuwaburudisha wasikilizaji.

Ndungo na Wangari (1991) wametoa maana ya hadithi kwa kuwaunga mkono, Hamad na wenzake, kwa kusema kwamba ni simulizi za kinathari. Lengo mahususi la kusimulia hadithi ni kuburudisha au kutumbuiza wasikilizaji au hadhira, kwa mfano wazee baada ya kumaliza shughuli za mchana kutwa, hukaa na watoto wao kuwasimulia hadithi kama ni sehemu ya kuwaburudisha watoto na kuwafurahisha. Hata hivyo, Wangari na Ndungo (wameshatajwa) wanaelezea, hadithi pia ina dhima ya kufundisha, kuonya au kuikosoa jamii. Kwahiyo utoaji wa maana ya hadithi na ufafanuzi mpana juu ya maana hiyo itasaidia kuongeza uelewa na ufahamu wa dhana hii kwa wale watakaotafitiwa kwa sababu imefafanuliwa vizuri.

### 2.2.1 Dhana ya Fasihi ya Watoto

(Wamitila 2002) anaeleza kwamba fasihi ya watoto, ni fasihi ambayo imekusudiwa watoto. Kwa maana hiyo ili kuhakikisha kuwa, fasihi hii imekuwa na mvuto kwa watoto, ni lazima fasihi hiyo iweze kufanikisha kuiteka saikolojia ya watoto. Anaendelea kusema kuwa, fasihi ya watoto ni fasihi maalumu, kwa ajili ya watoto. Maelezo haya ya Wamitila, yametupa ufafanuzi fulani, juu ya fasihi ya watoto, ambapo, ufafanuzi huo umetusaidia kupeleka mbele utafiti wetu huu, kwa mfano tumeweza kuzichambuwa hadithi kwa kuzingatia jinsi mtoto anavyojifunza kutokana na hadithi aliyosimuliwa au kusimulia, ingawa wao wanaelezea fasihi ya watoto iliyoandikwa lakini maelezo hayo angalau yametupatia muelekeo fulani unaohusu fasihi ya watoto. Hata hivyo, bado maelezo hayo hayajaweka wazi juu ya vipengele

muhimu ambavyo vinapaswa kuwemo katika fasihi ya watoto, na hasa katika dhamira za hadithi za watoto.

Wamitila (ameshatajwa) anasema kuwa, saikolojia ya watoto na vijana huwa na maana ya mambo yote, ambayo, yanakuwa katika kazi hiyo ili kuweza kuifanya kazi hiyo ya kuwavutia vijana. Ili kufanikisha kuiteka saikolojia ya watoto na vijana, mambo yafuatayo ni vizuri yaweze kuzingatiwa. Kazi hiyo,ni lazima iwe na mtazamo wa watoto na vijana ambao ni tofauti na watu wazima. Hivyo kufanikiwa kwa mwanafasihi, ni pale ambapo, kazi hiyo itaendana na fikra za watoto.

Kazi iwe na lugha rahisi inayoendana na hadhira ya watoto na vijana. Miundo mingine na sentensi ngumu hazipendekezwi kutumika katika fasihi ya watoto na vijana isipokuwa kama kuna ulazima wa kufanya hivyo, pia mwanafasihi anapaswa kuandika mada inayovutia watoto. Vile vile, mwanafasihi anapoiandikia hadhira ya watoto lazima hadithi yake iwe fupi na ya kiutendaji, kwani kazi ndefu huwachosha watoto, mwanafasihi anapowachora wahusika, lazima kuwachora kuwa na mhusika mwema na mhusika muovu kwani hali hiyo huwavutia sana watoto na kuwafunza, katika fasihi za watoto, wahusika wanyama wapewe nafasi za wahusika binaadamu kwani hali hii huwavutia watoto, kazi za watoto na vijana ni vyema ziwe za michezo, kwani, watoto hupenda sana michezo.

Maelezo hayo ya Wamitila (ameshatajwa) yamepiga hatua kubwa katika kueleza sifa bainifu zinazohusu hadithi za watoto. Maelezo hayo yametusaidia sana katika uchambuzi wetu, kwani yametupa mwanga wa namna ya kuzipata dhamira katika hadithi za watoto.

### 2.2.2 Dhana ya Fasihi Simulizi

Mulokozi (1996) kwa upande wake anatoa maana ya dhana ya fasihi simulizi kama ifuatavyo: Fasihi simulizi ni sanaa inayotungwa au kubuniwa kichwani nakuwasilishwa kwa njia ya mdomo na vitendo bila ya kuwepo kwa maandilizi. Kwa jumla tunapoangalia maana hiyo tutaona kwamba fasihi simulizi ni fasihi inayotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo na vitendo bila ya maandalizi yoyote kufanyika kabla ya kusimuliwa mbele ya hadhira iliyokusudiwa. Ni Fasihi ambayo haimfungi fanani katika kujiandaa pindi anapotamani kuiwasilisha kazi yake kwa hadhira.

Dhana hii ya fasihi simulizi nayo imefafanuliwa kwa sababu nayo imesaidia kusukuma gurudumu la mada hii ya tasnifu kwa sababu hadithi kwaujumla imetokana na fasihi simulizi au masimulizi ya mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwahiyo kupitia masimulizi hayo ndiyo tunapata hadithi ndani yake na kazi hii imejikita pia katika kusikiliza masimulizi hayo ya hadithi kwa ubora zaidi.

## 2.3 Maana ya Dhamira

Kwa mujibu wa (Sengo 2009), anaeleza kuwa dhamira ni sehemu ya maudhui, na maudhui ni yale yasemwayo na mwandishi wa kazi ya fasihi. Sengo (ameshatajwa), anaeleza kuwa dhamira ya mtunzi wa asili yaweza kuwa, ni mgogoro wa wanandoa, maandishi yakatoa dhamira kadhaa juu ya kugongana wenyewe kwa wenyewe, viongozi wa juu wa serikali, kutokusikilizana kwa vilabu vya mpira, shule na shule nakadhalika. Sengo (ameshatajwa), aghalabu, muhusika mkuu, hubeba dhamira kuu msemaji mkuu ni mwakilishi wa mtunzi. Kuna kazi ambazo humpa nafsi, huyo mtu aitwe “mpumbavu” kusema sema ya kipumbavu, kumbe hayo ndiyo kweli

aliyoikusudia mbunifu ama yale yanayodhihirisha na ubunifu wenyewe. Maelezo hayo ya Sengo juu ya dhana ya dhamira, yametupa uelewa mkubwa juu ya kuweza kuchambua dhamira katika hadithi za watoto. Maelezo hayo yamelenga moja kwa moja juu ya dhana ya dhamira. Maelezo haya kuhusu dhana ya dhamira inaonyesha ni uti wa mgongo ambao umesaidia kuufafanua utafiti wetu kwa maana umejikita kuelezea kwa kina zaidi lengo au dhumuni la hadithi mbalimbali za watoto wilayani Temeke

## 2.4 Mapitio mbalimbali kuhusu Hadithi

Utafiti kuhusu hadithi za Waswahili umefanywa na wataalamu mbalimbali ambao walikuwa na malengo tofautitofauti. Katika sehemu hii tutazungumzia kazi za wataalamu kadhaa ambao wamefanya kazi ambazo zina uhusiano na utafiti huu na kuona mchango wao katika utafiti huu mfano wa kazi hizo ni Semkiwa (1974), Dosha (2010), Nyamsende (2012), Mapunda (2012), Omary (2013), Ali (2015), Mzee (2015), Nyamsende (2015), Bwanga (2016), Omary (2021).

Semkiwa (1974) amekusanya hadithi tisa (9) za kienyeji maudhui ya kukusanya hadithi hizo ni kudumisha utamaduni, elimu, maarifa ya babu zetu na mawazo yao, katika hadithi hizo ameonyesha matumizi ya lugha jinsi yanavyowapa wanafunzi nafasi ya kuielewa na kuipenda lugha. Katika kazi hii mtafiti amepata mwelekeo wa kuikamilisha kazi yake ya utafiti kwa sababu nahau na methari zilizotumika zimesaidia katika uchambuzi na uibuaji wa dhamira.

Dosha (2010) aliangalia mchango wa hadithi katika kuendeleza mila na dasturi za Waha, katika Kata ya Muluhona, wilaya ya Kasulu. Lengo alilotilia mkazo ni

kutumia fasihi simulizi, kuifahamu kazi ya kisanaa ya jamii ya Waha, kwa lengo la kuimarisha sanaa hiyo ili iende na wakati. Katika hadithi alizozikusanya, aliibua maudhui na mafunzo ya kiuchumi pamoja na hali za maisha katika vipengele vya kifani kama vile muundo na mandhari. Mtafiti huyu, alikusanya hadithi kama vile Kisa cha mume na mke, Kisa cha mama wa kambo, Asiye sikia la mkuu, Wajinga ndio waliwao na Shibe mwana malevya. Kutokana na hayo, utafiti huo unaonekana kutoa mchango mkubwa kwa utafiti tulioufanya ambao unahusu kuchunguza dhamira katika hadithi za watoto mfano kutoka Wilaya ya Temeke.

Naye Nyamsende (2012) alitafiti utafiti wake unahusu usawiri wa taswira za wahusika wanyama katika ngano za Waikizu. Hadithi alizozikusanya, zinaonekana na ujumbe, kama vile ushauri mbaya, usitegemee bahati ya mwenzio, tenda wema uondoke, usiache mbachao kwa msala upitao, ukubwa wa pua si wingi wa makamasi. Pia, alionesha uchambuzi wa taswira za wahusika wanyama katika ngano teule, dhima na nafasi ya taswira za wahusika wanyama.

Hivyo basi, utafiti wa Nyamsende (keshatajwa) umetupa msaada mkubwa katika utafiti tulioufanya ambao umeangalia dhamira katika hadithi za watoto, kwani katika utafiti wake ameonesha vipengele vya kifani na kimaudhui, ambavyo kwa kiasi fulani, vimetuongoza katika utafiti huu hasa wakati wa kuchambua dhamira katika hadithi tulizozichagua kutoka Wilaya ya Temeke.

Mapunda (2012) aliangalia hadithi zilizosimuliwa kwa lugha ya Kinyiha. Mapunda (keshatajwa) alieleza dhamira zilizopatikana katika hadithi hizo za kabila la Wanyiha ambazo zimefasiriwakwa lugha ya Kiswahili na akagunduwa dhamira, falsafa,

mwelekeo na ujumbe. Dhamira alizogundua ni kama vile: Dhamira ya ukombozi, kuacha uchoyo, uzuri wa kufanya kazi na ubaya wa tamaa. Vile vile, alichambua vipengele vya fani kama vile matumizi ya lugha, muundo, mtindo, wahusika na mandhari. Kwa kutalii kazi hiyo mtafiti amepata mwelekeo na ufahamu mzuri wa kuzielewa dhamira mbalimbali na kufanya awe na uelewa mzuri katika utafiti wake alioufanya juu ya kuchunguza dhamira katika hadithi za watoto: mfano kutka Wilaya ya Temeke.

Omar (2013) alijadili nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema katika shule za upili visiwani Zanzibar.Alitafiti na kuainisha shida alizozipata mwanafunzi anayefundishwa maadili visiwani Zanzibar. Vilevile, alitafiti mbinu mpya za kufundisha hadithi simulizi katika kufunza maadili visiwani ambazo zingewawezesha Wazanzibari wengi kujifunza hadithi simulizi kwa urahisi. Tasnifu hiyo imesaidia katika kutuonesha jinsi ya kuzichambuwa hadithi na kutoa dhamira iliolengwa katika utafiti wetu huu ambao ni kuchunguza dhamira katika hadithi za watoto wilayani Temeke kwa sababu mtafiti huyo Omar (2013) amejadili jinsi ya kufundisha maadili yanayotokana na hadithi za fasihi simulizi hivyo katika utafiti tuliofanya mwandishi huyu amesaidia sana kwa kutuonyesha dhamira moja wapo ya masimulizi ya hadithi ambayo ni kufunza maadili mema kwa watoto na vijana ambayo ni moja ya uchunguzi wa dhamira katika hadithi za watoto wilaya ya Temeke.

Ali (2015) mtafiti huyu alifanya utafiti wa hadithi za fasihi simulizi zinavyomsawili muhusika mwanamke katika Hadithi simulizi za wapemba. Mtafiti Ali (ameshatajwa) aligundua kuwa hadithi simulizi za jamii ya wapemba zimemchora na

kumuweka katika nafasi mbalimbali. Hadithi hizo zimemsawiri mwanamke kama, mshauri, mzinzi, mtu mwenye tamaa, mbunifu, mlezi wa familia na mchapakazi.

Utafiti wa mtafiti Ali (ameshatajwa) pamoja na kuwa na lengo tofauti na utafiti huu, bado upo mfanano mkubwa kati ya kile alichokitafiti na hiki ambacho mtafiti wa kazi hii ametafiti, hivyo kupitia utafiti wa Ali (ameshatajwa) umemuongezea mtafiti wa kazi hii uelewa na ubunifu zaidi katika kazi yake ili kufikia malengo ya utafiti huu.

Mzee (2015) aliangalia maudhui yanayopatikana katika hadithi za watoto katika jamii ya Wapemba. Mzee (ameshatajwa) alielezea dhamira zilizopatikana katika hadithi za watoto katika jamii ya wapemba kama vile, dhamira ya mapenzi na ndoa, uhalifu, umoja na mshikamao. Vilevile alichambua vipengele vya fani kama vile wahusika, matumizi ya lugha, tamathari za semi, mandhari. Kwa kutalii kazi hiyo mtafiti amepata mwelekeo na ufahamu mzuri wa kuzielewa dhamira mbalimbali na kumsaidia awe na uelewa mzuri katika utafiti wake alioufanya juu ya kuchunguza dhamira katika hadithi za watoto mfano kutoka wilaya ya Temeke.

Nyamsende (2015) katika utafiti wake wenye mada "Ushujaa wa ushujaa wa motifu za safari na msako katika ngano za Waikizu, Wabondei na Wazanzibar," alitoa hitimisho kuwa kuna tofauti za falsafa na kaida za jamii hizi ndizo hufanya mashujaa wa hadithi hizo kutofautiana, mfano Nyamsenda (ameshatajwa) anasema kuwa katika jamii Kama ya Waikizu kama shujaa hatarajii kurudi nyumbani, basi huyo si shujaa. Kwa sabau shujaa wa ushujaa hudhihirika anaporejea nyumbani na asipo rudi basi huyo ameiacha asili. Nyamsenda (ameshatajwa) anaendelea kusema kuwa upo

utofauti wa shujaa kwa mfano, shujaa wa jamii ya Waewe ambapo shujaa anaweza kuondoka na asirudi. Pamojana tofauti hizo bado kunamuingiliano wa hadithi hizo.

Licha ya utafiti huu kuwa na utofauti na utafiti uliofanyika kutokana na kupishana kwa malengo kati ya tafiti hizi, mtafiti amegundua kwamba utafiti huo umefanyika daraja la manufaa katika kufikia lengo la utafiti huu kwasababu utafiti huo umeangalia kipengele cha wahusika ambacho ni kati ya vipengele ambavyo mtafiti katika utafiti huu ametafiti kupitia masimulizi ya hadithi kuna wahusika mbalimbali ambao wametumika kuelezea dhamira mbalimbali kutoka katika hadithi zilizokusanywa.

Bwanga (2016) mtafiti huyu naye alichunguza dhamira ya malezi inavyosawiriwa na wahusika mama wa kambo katika hadithi simulizi Zanzibar, kupitia utafiti wa mtafiti huyu umefanyika daraja na kutupa mwelekeo katika kufikia malengo ya utafiti huu. Mtafiti ameweza kuonyesha ni kwa namna gani dhamira zinavyoweza kuibuliwa katika hadithi  simulizi mfano wa hadithi hizo ni kama; “hadithi ya Mize na mama wa kambo”, “Sania na mama wa kambo”, “hadithi ya Mswamize na Rashidy”, kwahiyo hii itasaidia katika utafiti tunaotafiti.

Omary (2021) alitafiti vipengele vya fani jinsi vinavyoibua dhamira katika masimulizi ya ngano kisiwani Pemba. Omary (keshatajwa) alivitaja vipengele hivyo vya fani Kama wahusika, nao aliwagawanya katika makundi tofauti tofauti kama wahusika wanyama, majini, mazimwi, binadamu na wengine, vipengele vingine vya fani alivyotafiti ni mtindo, mandhari na matumizi ya lugha kwahiyo kupitia vipengele hivyo vya fani vilipelekea kuibua dhamira katika masimulizi ya ngano za

kipemba. Baadhi ya dhamira hizo ni kama; ujasiri, malezi, uongozi mbaya, utu, uchoyo, nafasi ya mwanamke, uhalifu na umaskini. Kwa kutalii kazi hiyo mtafiti amepata mwelekeo, uelewa na mwanga mzuri katika utafiti wake alioufanya juu ya kuchunguza dhamira katika hadithi za watoto mfano kutoka wilaya ya Temeke.

## 2.5 Pengo la Utafiti

Kwa kuangalia mapitio mbalimbali tunaona kuwa, jitihada zimekuwa kubwa katika kumzungumzia hadithi katika aina mbali mbali ambazo anazitumia mwanadamu katika maisha yake kwa ujumla akiwa mtoto. Hata hivyo, mbali ya tafiti nyingi ambazo zimefanywa, ni dhahiri ya kwamba mtafiti hakuona utafiti uliowahi kufanyika ukiwa na lengo la kuchunguza dhamira zinazo patikana katika hadithi za watoto: mfano kutoka wilaya ya Temeke. Hivyo basi, katika utafiti huu tunanuia kuchunguza dhamira zinazopatikana katika hadithi za watoto katika Wilaya ya Temeke ili kuziba pengo la kitaaluma katika fasihi ya Kiswahili. Maelezo tulioyaeleza katika aya zilizopita, tumeona kwamba watoto wamo ndani ya jamii na wanayo nafasi ya kubwa ya kujifunza mafunzo mbali yanayohusu jamii zao ili kuweza kuishi katika ustawi bora zaidi bila kukiuka taratibu zilizomo katika jamii husika. Katika utafiti huu mtafiti analenga zaidi kuchunguza dhamira zinazopatikana katika hadithi za watoto katika wilaya ya Temeke na namna ambavyo dhamira hizo zinavyoakisi jamii.

## 2.6 Mkabala wa Kinadharia

Wamitila (2008) anafafanua; Nadharia ni maarifa ya kitaaluma ambayo msomaji au mhakiki anapaswa kuyajua na kuyafahamu kabla ya kuianza kazi yake. Haya ni maarifa ambayo inatupasa kuwa nayo kabla ya kujihusisha na kazi ya uhakiki. Ni

maarifa ambayo yatamwezesha msomaji pia kuyaelewa mambo muhimu, na kwa njia hiyo, kuuboresha usomaji wake na uwezo wake wa kuifurahia fasihi. Maarifa haya yote ni sehemu ya Nadharia ya Fasihi.

### 2.6.1 Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi

TUKI (2004) inaeleza kwamba nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ni taaluma ya kisayansi inayohusu asili na maendeleo ya jamii sambamba na tabia zake, nadharia hii chimbuko lake ni nchini Urusi na imeasisiwa na George Lukacs (1916). Hutazama kazi ya sanaa kwakuzingatia hali ya jamii inamozaliwa na kukuzwa sanaa hiyo. Kazi hii imetafitiwa kwa kutumia nadharia hii ya Sosholojia ya Fasihi tunaamini imetuongoza kufikia lengo la utafiti huu. (Coser, 1963) anaeleza kwamba, Sosholojia ya Fasihi ni kitengo maalumu cha uchunguzi ambacho humulika mahusiano baina ya kazi ya sanaa, umma na muundo wa kijamii na jinsi kazi hiyo imejitokeza na kutathminiwa ubora na uhafifu wake. Masuala yanayojitokeza katika jamii yanayohusiana na uundaji wa kazi za fasihi kwa sehemu kubwa hutegemea jinsi mwandishi anavyohusiana na jamii yake kwa maana kila kinachotokea katika kazi ya fasihi huwa ndo kina akisi  jamii husika hivyo ni ngumu sana kuitenga kazi ya fasihi na jamii ambamo kazi hiyo imechipukia au kuanzia.

Hunuia kueleza sababu ambazo zimechangia kuibuka kwa kazi ya sanaa iliyo na umbo la kijamii na jinsi fikra za ubunifu wa mwandishi huongozwa na mila, desturi na mpangilio wa jamii husika. (Coser, 1963) anaeleza kuwa binadamu ndiye kiumbe pekee mwenye uwezo wa kutumia lugha kwa miaka mingi iliyopita binadamu amekuwa akijishughulisha na ukusanyaji wa maarifa pamoja na kanuni za mwenendo maishani.

Mungah (1999) anasema kwamba mtu anayefahamika kama muasisi wa nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ni Hippolyte Taine (1828-1893) katika kitabu chake cha History of English Literature (1863) aliitafiti kazi ya fasihi kama taswira ya kijiografia, kimazingira na kiutamaduni hutoka katika jamii husika, kazi ya fasihi huwa katika uhalisia na ukweli na jamii husika hivyo basi kupitia nadharia ya sosholojia ya fasihi kuna uhusiano wa dhati kati ya kinachotokea katika jamii na kinachoandikwa. Mihimili ya nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ni kama ifuatavyo:

Umahsusi na sio umajumui; Nadharia hii ilikuwa mahsusi zaidi kuliko nadharia zilizotangulia: badala ya kujikita katika taaluma ya sanaa jadi kwa ujumla (maumbile ya mwanadamu na utamaduni wa mwanadamu) kama walivyofanya wanadharia wa zamani nadharia ya sosholojia ilijikita katika jamii peke yake. Baada ya kugundua dosari zilizofanywa hapo awali; dosari za kutoa matamko ya juu juu na ya kijumla zaidi, kauli hizo ziliitupilia mbali mbali vipengele fulani vya maisha na mienendo mingine kwahiyo tofauti hizo ziliitofautisha jamii moja na nyingine hivyo wanasosholojia waliazimia kuchunguza kila jamii kwa wakati na nafasi yake kwa kurekodi kila kilichopatikanakatika jamii husika yani sanaa jadi yao.

Nadharia hii inaamini binadamu ni uti wa mgongo wa ulimwengu wa sanaa kwaujumla, kwahiyo kazi yoyote ya fasihi ni taswira ya kijiografia, kimazingira na utamaduni ambapo ndipo kazi hiyo imeanzia hivyo kazi hiyo haipaswi kutenganishwa na muktadha wa jamii ambapo ndimo imeanzia.

Msisitizo juu ya dhima ya Fasihi Simulizi; Tofauti na ilivyokuwa inadhaniwa hapo mwanzo kuwa Fasihi Simulizi ni mabaki tu ya zamani na kwamba hayakuwa na

umuhimu wowote katika maisha ya jamii katika zama za kisasa, wanasosholojia waliamini kuwa uamilifu wa fasihi simulizi upo hai na haufi na kwamba unabadilika kulingana na maendeleo ya jamii husika na fasihi ina dhima kubwa kwa jamii kama vile kuelimisha jamii kuburudisha jamii na kukemea maovu yasiyofaa katika jamii, kusuluhisha migogoro inayotokea katika jamii ili kuleta usawa katika jamii.

Mkazo katika utendaji; Tofauti na ilivyokuwa wananadharia wa nadharia zilizotangulia ambao hawakupendelea kusoma na kuiishi fasihi simulizi, wanasosholojia ya jamii waliweka msisitizo zaidi katika kuchunguza watendaji wa fani mbalimbali za kifasihi kutokana na msisitizo wao huo imebainika kuwa, Fanani wa fasihi simulizi wanaujuzi na ustadi wa kiutendaji katika sanaa husika yani ubunifu wao ni mkubwa sana na wamesaidia kusogeza mbele katika kuielewa fasihi simulizi.

Muktadha wa kazi ya Fasihi; Katika nadharia hii ya sosholojia ya fasihi moja ya muhimili wake ni kuwa mhakiki wa kazi ya fasihi hawezi kuhakiki kazi yoyote ile pasipo kuzingatia muktadha wa mazingira na maisha ya mwandishi huyo, kwahiyo si kazi ya fasihi inayochunguzwa bali pia vipengele vilivyo nje ya kazi hiyo.

Kwa hakika kila nadharia huwa na umuhimu na yenye ubora na mapungufu yake. Uteuzi wa nadharia bora itategemea uteuzi wa mtafiti kwa mujibu wa mada, malengo na maswali ya utafiti wake. Kutokana na hali hiyo mtafiti amekusudia kutumia nadharia ya Sosholojia ya fasihi. Msingi mkubwa wa kuchagua nadharia hii ni imani ya mtafiti ya kwamba nadharia hii inaweza kufanikisha vyema na kwa kiwango cha

juu malengo na maswali ya utafiti huu ambayo ndio roho kuu ya utafiti huu. Nadharia hii imechambuliwa vyema ikihusishwa na misingi/mihimili yake.

## 2.7 Hitimisho

Katika sura hii tumefanya mapitio ya kazi tangulizi na kubaini kuwa utafiti kuhusu kuchunguza dhamira katika hadithi za watoto: Mfano kutoka wilaya ya Temeke ulikuwa bado haujafanywa na mtafiti mwingine. Hivyo, tumeona kuwa hili ni pengo la kimaarifa ambalo kwa kuliziba tumetoa mchango wetu katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili. Pamoja na hayo, katika sura hii tumewasilisha nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ambayo ndiyo imetumika katika kuchambua data za utafiti. Sura ifuatayo mtafiti amewasilisha vipengele na mbinu za utafiti zilizotumika.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa Kothari (2004) mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Sura hii imechunguza njia za utafiti zilizotumika katika mchakato wa utafiti. Njia hizo huonesha namna mtafiti alivyokusanya, alivyozichambua na kuziwasilisha data kwa kuziandikia taatifa ya utafiti (Mligo, 2012). Katika sehemu hii vipengele vitakavyo shughulikiwa ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, vyanzo vya data, watafitiwa, mbinu za ukusanyaji data, uchambuzi wa data na kuaminika kwa data. Mbinu hizo zilimsaidia mtafiti katika ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa data zilizomwezesha kufikia malengo ya uchunguzi uliofanyika.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni sehemu ambapo mtafiti hulenga kutafuta data zake kwa ajili ya kukamilisha malengo mahsusi ya utafiti wake (Gupta & Gupta, 2011). Eneo la utafiti huteuliwa kulingana na lengo kuu la utafiti. Utafiti huu ni wa uwandani. Data za msingi zimepatikana katika kata ya Kijichi, Mbagala, Mtoni, Temeke na Chamanzi. Kata hizo zilikuwa muafaka kupata data za msingi zilizokusudiwa katika utafiti uliofanyika. Data za upili kwa ajili ya kurejelea data za msingi zimepatikana kwa kudurusu machapisho mbalimbali mtandaoni na maktabani. Baadhi ya maktaba zilizohusika ni maktaba kuu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania iliyopo Dar es Salaam.

### 3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mpangilio unaoonesha sura nzima ya uchunguzi unavyopaswa kufanyika kuanzia katika hatua ya ukusanyaji wa data mpaka hatua za uandishi wa taarifa ya utafiti (Franklin, 2012 & Mgogo, 2017). Mpango huo huonesha kuwa utafiti unaohusika utakuwa ni wa namna gani na jinsi data zitakavyokusanywa. Mbinu ya uchunguzi kifani imetumika katika utafiti huu. Mbinu hii humpa fursa mtafiti kuteua eneo mahsusi aliloshughulikia katika utafiti wake. Uchunguzi kifani katika utafiti huu ni kata ya Kijichi, Mbagala kuu, Mtoni, Temeke na Chamanzi. Uteuzi huo ulimwezesha mtafiti kupata na kutumia muda muafaka wa kukusanya data nyingi za kutosha kukamilisha utafiti wake.

### 3.4 Vyanzo vya Data

Utafiti huu ulikuwa ni wa uwandani. Data za msingi katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika kata ya Kijichi, Mbagala Kuu, Mtoni, Temeke na Chamanzi. Data za msingi ni zile ambazo hazijawahi kukusanywa na mtu mwingine kwa wakati huo (Cryer, 2000 & Robert, 2009). Kata teule zilitupatia data zilizotusaidia kukamilisha malengo mahsusi ya utafiti huu. Pia, mtafiti alidurusu data za upili kwa ajili ya kuthibitisha na ufafanuzi wa data za msingi kutoka mtandaoni na maktabani. Ili kupata data zilizotakiwa, mtafiti alilazimika kusoma machapisho mbalimbali katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania iliyopo Dar es Salaam.

### 3.5 Kundi Lengwa

Walengwa hutazamwa kama washiriki wote, binafsi au kundi ambalo mtafiti hulitumia kwenye utafiti wake. Walengwa ni sehemu ya watu au vitu vinavyotarajiwa kumpatia mtafiti data za utafiti ili aweze kutimiza malengo mahsusi

ya utafiti anaokusudia (Bernard, 2000; Israel & Hay, 2006). Katika utafiti huu, mtafiti ametumia kundi lengwa ili kupata data za msingi. Utafiti huu umeshirikisha watafitiwa (50) wenye mchanganuo kama ufuatao, katika kila kata kuna watu kumi (10). Ambapo katika kila kata inakuwa na idadi ya watoto (5) ambao ni wanafunzi wa darasa la nne mpaka la saba (tumetumia wanafunzi wa darasa la nne mpaka la saba kwa sababu tunaamini ni watoto ambao wamejielewa na wameshasoma hadithi na watu wazima (5) Mgawanyo huu umesaidia kuweza kupata data za uhakika kutoka kwa walengwa. Hata hivyo sababu iliyotupelekea kuteua watafitiwa hao ni kutokana na sifa, ujuzi, na kuwa na upeo wa kutosha katika hadithi za watoto. Pia taarifa hizo zimepatikana katika makazi halisi ya watafitiwa. Kwa kutumia usampulishaji lengwa mtafiti ameweza kuwapata watafitiwa wake katika eneo la utafiti, na kuanza kufanya nao majadiliano, katika makazi yao (shuleni na nyumbani). Mbinu hii imefaa sana kutumika katika utafiti huu hasa kutokana na maumbile ya utafiti huu.

**Jedwali Na. 3.1 Jedwali la watafitiwa**

| NAMBA | JINA LA KATA | IDADI YA WATU WAZIMA | IDADI YA WATOTO | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | KIJICHI | 5 | 5 | 10 |
| 2 | MTONI | 5 | 5 | 10 |
| 3 | MBAGALA KUU | 5 | 5 | 10 |
| 4 | TEMEKE | 5 | 5 | 10 |
| 5 | CHAMANZI | 5 | 5 | 10 |
| | JUMLA | 25 | 25 | 50 |

### 3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data ni hatua moja muhimu sana katika utafiti, mtafiti kabla ya kuanza kukusanya data alipaswa kujua aina gani ya data alizo zihitaji kukusanya na ni kwa kiasi gani cha upeo ulio muwezesha kuamini kuwa data alizozikusanya zilitosha kukamilisha utafiti wake. Vile vile ukusanyaji wa data ni njia ya pekee ya kutafuta taarifa mbalimbali zenye ukweli ndani yake (Kombo na Tromp 2006). Ziko mbinu mbalimbali za ukusanyaji data na kila mbinu ina ubora na udhaifu wake katika kukusanya data za utafiti. Utumiaji wa njia zaidi ya moja humwezesha mtafiti kupata, kuthibitisha, kuhakiki na kurekebisha data alizozikusanya. Mbinu hizi huzifanya data ziweze kuaminika kwakiasi kikubwa. Mtafiti ametumia mbinu ya ushuhudiaji, mbinu ya usaili na mbinu ya maktabani. Mbinu hizo ni:-

#### 3.6.1 Ushuhudiaji wa Utambaji Hadithi

Ushuhudiaji ni njia mojawapo ya mbinu katika ukusanyaji wa data ambayo mtafiti aliitumia katika utafiti huu. Katika njia hii mtafiti hulazimika kwenda katika eneo husika na kushuhudia kile atakachokitafiti (Mulokozi, 2010). Katika mbinu hii mtafiti alifika shuleni na katika makazi ya wasailiwa watu wazima alishuhudia kikamilifu jinsi hadithi zilivyosimuliwa na yeye kusikiliza, kurekodi na kuchagua masimulizi ya hadithi kwa watafitiwa, ili kuweza kusikia na kujionea mwenyewe ishara na vitendo vinavyofanyika katika usimulizi wa hadithi hizo sambamba na kuimba nyimbo zilizokuwemo ndani ya hadithi husika. Aidha, mbinu ya ushuhudiaji ilitumiwa kwa lengo la kumsaidia mtafiti kupata taarifa sahihi ambazo ziliendana na malengo mahsusi ya utafiti huu. Maelezo zaidi yapo katika Kiambatanisho namba 1.

### 3.6.2 Dodoso

Dodoso inatokana na neno dodosa ambalo lina maana ya kudadisi mtu kwa kumuuliza maswali (TUKI, 2004). Katika utafiti huu, mtafiti ametumia dodoso kwa watoto na watu mbali mbali ambao wanaozisikiliza hadithi hizo. Mtafiti amewauliza kuhusu dhamira na jumbe zinazopatikana katika hadithi hizo. Mbinu hii ya dodoso imeweza kumsaidia mtafiti kujua hadithi mbalimbali pamoja na dhamira baada ya kusimulia tunapata dhamira na ujumbe gani? Pia mbinu hii imeweza kumnufaisha mtafiti kwa sababu ameweza kupata dhamira na ujumbe tofauti tofauti katika hadithi moja. Maelezo zaidi yapo katika Kiambatanisho namba 2.

### 3.6.3 Upitiaji wa Kinyaraka

Katika mbinu hii ya upitiaji wa nyaraka, mtafiti ametumia mbinu ya uchambuzi matini kukusanya data na taarifa mbalimbali. Kothari (1992:110) anaeleza kuwa uchambuzi wa matini ni njia ya kukusanya data kutoka katika vitabu, makala na matini za kielektroniki kwa lengo la kuzifanyia uchambuzi. Data zitazokusanywa kutoka vyanzo hivyo huitwa data fuatizi. Mtafiti ametumia mbinu hii kwa kusoma vitabu, makala na tovuti mbalimbali zilizokuwa zinahusiana na utafiti wake.

## 3.7 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kitendo cha kupangilia taarifa kwa namna ambayo data zilizopatikana husaidia kujibu maswali ya utafiti (Kothari, 2008). Uchambuzi wa data hufanywa kwa kuongozwa na mbinu zinazokubaliwa na kufaa kwa ajili ya kazi inayoshughulikiwa. Uchambuzi wa data humrahisishia mtafiti kuelewa mantiki ya kazi inayochunguzwa. Baada ya kukamilika kwa zoezi la ukusanyaji wa data zilizopaswa, mtafiti hutakiwa kuzichambua, kuzijadili na kuziwasilisha kwa

utaratibu mahsusi. Kwa msingi huo, uchambuzi wa data ni hatua muhimu katika kutimiza malengo ya utafiti. Mbinu ya kimaelezo na mkabala wa kidhamira zimetumika katika uchambuzi wa data katika utafiti huu.

### 3.7.1 Mbinu ya Kimaelezo

Uchambuzi wa data katika utafiti huu uliongozwa na mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo. Mbinu hii hutumika kuchambua data kwa mfumo wa maelezo bila kufuata taratibu za kitakwimu (Booth, 2003). Mbinu ya kimaelezo humruhusu na kumpa fursa mtafiti kuvielewa vipengele vinavyoshughulikiwa katika kazi inayochunguzwa. Katika utafiti huu, mtafiti alipata fursa ya kuzichunguza hadithi za watoto kwa undani kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti. Data zilikusanywa na kubainishwa katika makundi kulingana na malengo mahsusi. Hatua ya mwisho ilikuwa ni kuzijadili na kuziwasilisha data za utafiti uliofanyika kwa kuzitolea maelezo ya kina.

### 3.7.2 Mkabala wa Kidhamira

Mkabala wa kidhamira hutumika kuhakiki kazi za fasihi. Mkabala huu hutumika kuichambua kazi ya fasihi kwa kuzingatia hatua kuu nne (Leary, 2001). Hatua ya kwanza, ni kukusanya data zilizolengwa. Pili, kuoanisha mada na data zinazohusika. Tatu, kupangilia data kimantiki kwa kuhusianisha dhamira kuu na dhamira ndogo ndogo. Nne, kuandaa vipengele vilivyozingatiwa katika uchambuzi wa data. Ili kukamilisha malengo ya utafiti uliofanyika, mtafiti alizingatia hatua zote nne za mbinu ya uchambuzi wa kidhamira. Katika hatua ya kwanza na ya pili, data za utafiti zilikusanywa na kuoanishwa na mada ya utafiti. Hatua ya tatu, data zilipangwa ili uchambuzi ulingane na malengo mahsusi ya utafiti. Hatua ya nne, uchambuzi wa

data ulifanyika kwa namna iliyokamilisha malengo ya utafiti. Machapisho yaliyopitiwa yalinukuliwa pale ilipobidi ili kuthibitisha na kujaziliza uchambuzi wa data za msingi na nadharia.

## 3.8 Kuaminika na Ubora wa Data

Kuaminika kwa mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data ni utaratibu unaowezesha kupatikana kwa data za kuaminika, halali na bora (Saunders, 2007 & Berg, 2009). Kuaminika kwa data za utafiti kutokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa matokeo yale yale pindi utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zile zile. Katika utafiti huu, mtafiti alikusanya data kwa mbinu ya hojaji, shirikishi na usaili na ile ya uchambuzi wa nyaraka. Aidha, uchambuzi wa data uliongozwa na nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Mbinu za kimaelezo na kidhamira zilitumika katika uchambuzi na uwasilishaji wa data zilizochunguzwa. Kwa msingi huo, upungufu wa mbinu moja ulikamilishwa na ubora wa mbinu nyingine. Mjadala kuhusu uhalali na ubora wa mbinu zilizotumika ulifanyika kati ya mtafiti, msimamizi wake pamoja na wanataaluma wengine wa fasihi ya Kiswahili katika ngazi ya uzamili. Aidha, kuaminika kwa data katika utafiti huu kulithibitishwa kwa kutumia nadharia zilizoongoza mjadala wa data, mbinu za ukusanyaji wa data, njia za uchambuzi na uhakiki wa data zilizowasilishwa katika utafiti huu.

## 3.9 Itikeli ya Utafiti

Utafiti wa kitaaluma una maadili yanayopaswa kuzingatiwa kikamilifu. Maadili ya utafiti huzingatia kanuni, sheria na miongozo iliyowekwa katika utaalamu fulani (Cohen, 2000). Hali hii hujitokeza kwa kuwa watafiti hawana mtazamo na fikira za aina moja katika utendaji wa kazi zao za kiuchunguzi. Huu ndio msingi wa Hakimu

(2000) kuona umuhimu wa kuwapo kwa kanuni na mambo ambayo yatatumika kuwaweka watafiti wote katika uwiano fulani utakaowaongoza katika kulishughulikia jambo ambalo ni sahihi au lisilo sahihi katika mchakato mzima wa utafiti.

Katika uchunguzi wetu, masuala ya kiitikeli yamezingatiwa kikamilifu. Masuala ya yaliyohusika katika utafiti huu ni namna mtafiti alivyoweza kuzingatia maadili ya utafiti kabla, wakati wa ukusanyaji wa data na wakati wa uandishi wa taarifa ya utafiti.  Masuala ya kimaadili ambayo yanapaswa kuzingatiwa katika utafiti ni pamoja na umuhimu wa usiri, ushiriki wa hiari bila watafitiwa kulazimishwa, kupata ruhusa ya kufanya utafiti katika maeneo yaliyokusudiwa (Baxer & Wenzake, 2001). Kwanza, mtafiti alipata kibali cha kukusanya data kwa kufuata mwongozo wa Chuo. Mtafiti alipata barua kwa Mkurugenzi wa Elimu ya Juu wa Chuo Kikuu Huria ili kumtambulisha na kudhihirisha haki za kisheria za kiutafiti. Kibali hicho kilimsaidia mtafiti kurahisisha shughuli ya utafiti katika maeneo ambayo alikwenda kukusanya data zilizokusudiwa.

Pili, katika utafiti wa kisayansi, mtafiti hatakiwi kuegemea upande wowote katika hatua za utafiti na kutoa taarifa sahihi, bora na za kuaminika ili kukamilisha utafiti wake. Aidha, kuegemea upande mmojawapo kuhusiana na matokeo ya utafiti ni kinyume na maadili ya taaluma ya utafiti. Kwa hiyo, mtafiti anapaswa kutoa taarifa kwa usahihi, bora na zenye kuaminika kwa kufuata taratibu za utafiti wa kitaaluma (Charkrabarthy, 2012). Katika utafiti huu wa uwandani, mtafiti aliandaa na kuandika taarifa ya utafiti kulingana na data za msingi zilizopatikana katika hadithi teule kwa

kurejelea baadhi ya maandiko mengine yaliyowiana na mada ya utafiti iliyokuwa imelengwa.

Kwa ujumla, maadili ya utafiti yalimhusu mtafiti na mahusiano yake na katika mchakato wa utafiti tangu hatua ya ukusanyaji wa data, uchambuzi, mjadala na wakati wa uandishi wa ripoti. Jambo la kuzingatiwa katika mchakato huo ni kuhakikisha kwamba, mtafiti hawi kiini cha kubetua data za msingi wakati wa uandishi wa taarifa ya utafiti. Kwa upande mwingine, mtafiti au watafitiwa hawatakiwi kuathiriwa kwa namna yoyote kisaikolojia na kimwili kutokana na kushiriki kwao (Furlong, 2000). Kwa hiyo, itikeli ya utafiti imezingatiwa kikamilifu ili kuhakikisha uchunguzi umefuata misingi ya kisayansi na taaluma ya utafiti.

### 3.10 Hitimisho

Katika sura hii, mbinu za utafiti zimewasilishwa. Baadhi ya vipengele vilivyoshughulikiwa katika sehemu hii ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, vyanzo vya data, watafitiwa, mbinu za ukusanyaji wa data, mbinu za uchambuzi wa data, kuaminika na ubora wa data na itikeli ya utafiti. Mbinu hizo zimemuongoza mtafiti katika mchakato mzima wa utafiti huu. Mbinu hizo zimetegemeana na kukamilishana katika hatua zote za utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti hufanywa pale tu data za utafiti zinapokuwa tayari zimeshakusanywa na kupangiliwa vizuri kwa namna ambayo inasaidia kujibu maswali ya utafiti. Hii ni hatua muhimu katika utafiti kwa sababu ndiyo inayokusudiwa ibainishe matokeo ya utafiti na kutatua tatizo la utafiti. Hivyo, uchambuzi wa data za utafiti huu umefanywa kwa kurejelea malengo mahususi ya utafiti huu ambayo yalikuwa ni kuchambua dhamira katika hadithi za Watoto katika wilaya ya Temeke na lengo la pili ni kubainisha ujumbe unaojitokeza katika hadithi za watoto wilaya ya Temeke. Katika uchambuzi wa data za utafiti huu tumechambua malengo yote mawili kwa pamoja kwa kutumia hadithi 22 tumeanza na data zinazohusiana na lengo mahususi la kwanza na kisha lengo mahususi la pili. Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi imetumika katika uchambuzi wa data za ufati huu.

## 4.2 Maana ya Dhamira na ujumbe katika kazi ya Fasihi

Dhamira ni mojawapo kati ya vipengele vinavyounda maudhui katika kazi ya fasihi huku vipengele vingine vikiwa ni migogoro, ujumbe, falsafa, msimamo na mtazamo wa mwandishi (Njogu na Chimerah, 1999). Wamitila (2008) anaeleza kuwa dhamira ni yale mawazo makuu ambayo yamemsukuma mwandishi wa kazi ya fasihi kuyaandika na yanajibainisha vizuri katika kazi husika. Kezilahabi (2003) anaiona dhamira kuwa ni lengo kuu la mtunzi wa kazi ya fasihi ambalo analilenga liifikie hadhira aliyoiteua. Mtaalamu huyu anakwenda mbali zaidi na kueleza kuwa si kila mtu anaweza kuwa ni hadhira ya kazi fulani ya fasihi kwa sababu kila mwandishi

huandika kazi yake akiwa na lengo kuu ambalo anataka hadhira yake ilipate. Hilo lengo kuu ndilo ambalo linafahamika kama dhamira ya mwandishi.

Dhamira ya mwandishi kwa kawaida hugawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni dhamira kuu na dhamira ndogo ndogo. Dhamira kuu ni ile ambayo inakuzwa na kujitokeza katika kazi nzima ya fasihi na dhamira ndogondogo ni zile ambazo zipo kwa ajili ya kuikamilisha dhamira kuu. Watunzi wa hadithi za watoto zimesheheni utajiri mkubwa wa dhamira na mafunzo kwa jamii. Dhamira zilizojitokeza katika hadithi hizi za watoto wilaya ya Temeke ni ni nyingi lakini katika utafiti huu tumeteua dhamira za usafi wa mazingira, mapenzi katika jamii, wizi, umasikini, malezi, ujasiriamali.

Ujumbe ni mafunzo yanayopatikana baada ya kusoma au kusikiliza na kupitia kazi fulani ya kifasihi ujumbe unaweza kutolewa kwa njia mbalimbali kati ya mtu na mtu, lakini pia kwa umati hasa siku hizi kupitia vyombo vya mawasiliano ya kijamii. https://sw.m.wikipedia.org (4.Novemba.2023)

### 4.2.1 Usafi wa Mazingira

Mazingira ni jumla ya vitu na mambo yote ambayo yanamzunguka mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. Vitu na mambo hayo yanayomzunguka mwanadamu ni pamoja na milima, mabonde, mito, bahari, miti, majani, wanyama pori, makazi, taasisi za elimu, afya, utawala wa kiserikali, dini, mila na desturi na maziwa kutaja kwa uchache (Skeggs, 1997). Vitu hivi vyote vinayo nafasi kubwa katika kumfanya mwanadamu aweze kuishi maisha ya amani na utulivu na yenye afya kamili. Pamoja na ukweli kuwa mazingira ni vitu ambavyo vimemzunguka mwanadamu lakini pia

naye mwanadamu ni sehemu ya mazingira hayo. Mwanadamu anao uwezo wa kuyastawisha au kuyaangamiza mazingira kwa njia mbalimbali. Pale anapoyaimarisha mazingira ndipo mazingira hayo yanapokuwa na manufaa kwa mwanadamu huyo wa sasa na kizazi kijacho. Kwa mfano, ikiwa mwanadamu atadumisha mazingira katika kusafisha maeneno ambayo yanamzunguka itampelekea kuishi vyema na kuifanya miji kuwa yenye kupendeza. Kinyume chake, ikiwa mwanadamu kazi yake itakua kuacha uchafu uendelee kuzagaa katika miji itaendelea kuwa ni hasara kwa taifa kwani kwa kuongezeka kwa maradhi mbali mbali katika jamii na hata taifa kwa jamii.

Usafi wa mazingira ni jambo muhimu ambalo linaifanya jamii kuwa na afya njema au mbaya kama mazingira hayakusafishwa ipasavyo. Hivi leo katika mikoa mingi ya Tanzania kumeripotiwa kuwa na wagonjwa wengi wakiwemo wa kipindupindu, malaria yatokanayo na uchafu wa mazingira. Katika hadithi za watoto hadithi namba 4 ya “Sungura na Fisi” wilaya ya Temeke umebainishwa kuwa uchafu wa mazingira ni tatizo ambalo linaikabili jamii ya Watanzania kama ifuatavyo:

> “*Paukwa... Pakawa...*
> *Hapo zamani za kale walitokea watu wawili watu hao waliitwa Sungura na Fisi. Siku moja Sungura alienda nyumbani kwa Fisi na alikuta kuna nyasi nyingi Sungura alimuuliza, “Fisi mbona mazingira yako ni machafu sana? Fisi akajibu eeebwana mimi naumwa sana, nasumbuliwa na mgongo kwahivyo siwezi hata kuinama kusafisha mazingira yangu. Bwana Sungura akasema.”*

Katika kifungu hicho hapo juu inaonekana kuwa katika jamii kuna tatizo la uchafu wa mazingira kutokana na watu kutokuwa na tabia ya kufanya usafi katika maeneno yao. Uchafu kuzagaa katika nyumba pasi na kuzolewa kwa wakati na kupelekwa

sehemu ambazo zimetengwa maalumu, husababisha mlipiko wa magonjwa kama kipindupindu, kichocho, kuharisha na homa za matumbo. Watu wengi Tanzania wamejenga fikra vichwani mwao kuwa mwenye jukumu la kufanya usafi katika maeneo yao ni serikali na kusahau kwamba wao ndio wadau wa kwanza wa usafi katika makazi yao na mahala pa kazi.

Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi huamini kuwa fasihi ni zao la jamii na kinachozungumzwa katika kazi ya fasihi kina uhalisia na ukweli ndani yake na kinachotokea katika maisha ya jamii. Mfano katika jamii yetu ya Tanzania kuna sehemu watu hukaaa katika mazingira machafu na hawataki kufanya usafi mpaka wanapata magonjwa kama kuhara na kipindupindu, mhusika Fisi ameweza kuyaacha mazingira yake kuwa machafu kama jukumu lake la msingi katika maisha yake. Pamoja na imani ambayo ameionesha Sungura kwa rafiki yake haiingii akilini kwamba mtu binafsi ndiye anayetumia kila kitu katika nyumba yake na kuzalisha uchafu na taka halafu mtu mwengine ndio afanye usafi. Mtu wa kwanza kuwajibika na usafi wa mazingira ni yule mtu anayeishi katika mazingira husika.

Aidha, ujumbe ambao tunaupata katika hadithi hii ya sungura ni pamoja usafi wa mazingira ni jambo la lazima na la muhimu katika jamii zetu kila mtu aipende sehemu anayokaa au kuishi iwe pahala safi na salama, mapenzi ya dhati aliyokuwa nayo sungura kwa rafiki yake na mwisho kutowaamini wengine kwa wapo baadhi ya watu hawaaminiki katika maisha hata ukiwatendea wema wao bado wanatafuta njia ya kukudhuru. Mbali ya yote hayo, jambo la msingi, ikiwa kila mwananchi atajitahidi kufanya usafi katika eneo lake mazingira yatakuwa safi na magonjwa ya mlipuko yatatoweka kabisa.

### 4.2.2 Wizi

Wizi ni njia za kujipatia mali na fedha kutokana na biashara au kazi ambazo si halali kisheria. Kwa mfano, mtu au kikundi cha watu kinavamia nyumba ya mtu na kupora vitu vya thamani kama fedha, simu, kompyuta, televisheni na redio na kisha kujipatia utajiri kutokana na wizi huo. Pia, baadhi ya watu hufanya vitendo vya wizi kwa kutumia silaha na kuiba fedha katika mabenki na maduka ya wafanyabiashara na kujipatia utajiri ni mambo yasiyokubalika au baadhi ya wengine kuiba mazao ya wakulima na kuwaibia wafugaji hata wadogo wadogo. Baadhi ya watu hufanya wizi wa kughushi na wengine kuibia serikali au sehemu wanapofanyia kazi. Wizi wa aina hii huhusishwa pia na rushwa na ufisadi (Khamis, 2007). Kupitia muhimili wa nadharia hii unaamini fasihi ni zao la jamii lsenye kuelezea uhalisia na kuiakisi jamii ni kweli kabisa nadharia hii inaiakisi jamii kupitia dhamira ya wizi katika jamii. Mfano,

Katika nchi ya Tanzania jiji la Dar es Salaam kumekuwa na tatizo kubwa la wizi katika maeneo yote ambayo tumeyataja hapo kiasi ambacho wananchi na hata serikali wamekuwa wakisononeka na kusababisha kurejesha nyuma maendeleo ya taifa kwa ujumla pamoja na kutokea athari kubwa kwa wafanyao wizi huo kwa kuuwawa na kufungwa jela baada ya kesi kumalizika jambo ambalo linarejesha nyuma maendeleo ya Taifa pia (Diegner, 2011). Katika hadithi ambazo zimehadithiwa na watoto wilaya ya Temeke hadithi namba 3 ya “Kondo na Kuku” inatuonesha wizi huo kama ifuatavyo:

> *Hapo zamani za kale katika kijiji cha Gwata palitokea kijana aliyeitwa Kondo aliishi huko Bumbwi Alikuwa na tabia ya wizi na hakutaka kufanya kazi ilia pate ridhiki yake halali bali alitegemea kuiba na kupora vitu vya watu.Wanakijiji wa Gwata walichoka na*

> *tabia yake. Siku moja Kondo aliiba kuku wa jirani yake Chumu maeneo ya Bumbwi, alikamatwa hadi kituo cha polisi na baadae…..”*

Kifungu hiki cha maneno hapo juu kinaonesha kuwa wapo wanajamii wengi ambao wanaishi kwa kutegemea wizi. Hali hii imezoeleka na kuonekana kuwa ni kitu cha kawaida mtu kupata utajiri kwa kutumia njia zisizokubalika ndio maana kondo aliishi kwa kutegemea kuiba pasi kutaka kufanya kazi za halali ili aweze kujiapitia riziki za halali. Haya ni maneno yanayotoa ushahidi kuwa ile dhana ya kuwa utajiri hupatikana kutokana na watu kufanya kazi imetoweka na sasa watu wanatafuta utajiri kwa kutumia wizi. Hali hii inawafanya wanajamii kubweteka na kuamini kuwa ni kweli wizi ndio njia muafaka ya kuweza kuendesha maisha.

Mtaalamu wa masuala ya sosholojia (Ritzer, 2008) anaeleza kuwa mwanadamu ni mtu mwenye tamaa ya mali na kila mara hutaka kuwa ndiye mtu mwenye mali kulio wanajamii wote. Ili kuweza kutimiza tamaa yake hutafuta njia rahisi na ya mkato ambayo itaweza kumpatia utajiri wa haraka haraka. Kutokana na hali hii ndio maana baadhi ya watu hujiingiza katika vitendo vya wizi, ubadhirifu wa mali za umma, rushwa na ufisadi ili wapate mali za harakaharaka. Kwa mfano, tumeweza kumuona Kondo namna alivyo weza kupata madhara ya kwenda kutumikia mafunzo (jela) bila ya kutegemea na kubakia kwake majuto. Aidha, wapo watumishi wa serikali ambao wanaripotiwa mara kwa mara kuwa wanajipatia utajiri kwa njia ambazo sio halali na kulifanya taifa linaendelea kudidimia Sheria kali zinatakiwa kuchukuliwa dhidi ya watumishi wa aina hii ili iwe funzo kwa wengine (Cross, 2011).

Ujumbe tunaoupata kupitia dhamira hii ni kuwa tabia ya wizi ni tamaa pia sio nzuri mtu waweza kuishia pabaya mfano kuchomwa moto kwa sababu ya kuiba kitu hata

kidogo tu kitakutia matatizoni hivyo inatubidi kuridhika na chochote mtu ulichonacho.

### 4.2.3 Ujasiriamali

Ujasiriamali ni neno linalotokana na maneno mawili ambayo ni “jasiri,” na “mali.” Maneno haya yameunganishwa pamoja na kupata neno “ujasiriamali,” likiwa na maana kuwa ni kitendo cha mtu kuwekeza fedha au kitu chenye thamani ili aweze kupata faida zaidi kutokana na uwekezaji alioufanya. Mtu anayefanya kitendo cha ujasiariamali anajulikana kama mjasiriamali (Tonkiss, 2006). Huyu ni mtu ambaye haogopi kuwekeza kwa dhana kwamba hatapata faida na hivyo fedha au mali aliyowekeza itapotea. Mjasiriamali huamini kuwa uwekezaji atakaoufanya utamletea tija na kwamba na hata ikitokea haukuleta tija aliyotarajia atajitahidi kupambana ili kuufanya uwekezaji wake uwe imara na wenye tija. Huyu ni mtu jasiri kwani si kila mtu na si jambo jepesi mtu kuamua kufanya uwekezaji bila ya kuwa na hofu juu ya mustakabali wa uwekezaji wake huo ambao ni mpya (Anivery, 1970). Kwa hakika ujasiriamali ni dhana ambayo imekuwepo tangu enzi na enzi lakini imepata mashiko zaidi katika miaka ya mwishoni mwa 1990 mara baada ya kuanzishwa na kuruhusiwa kwa soko huria. Ujasiriamali ulionekana kuwa ni moja kati ya eneo ambalo linaweza kutoa ajira kwa watu wengi wakiwemo wanaume na wanawake.

Ni ukweli usiopingika kuwa, wajasiriamali hupata tabu katika kutafuta kwao ingawaje wanaendelea kupambana, mfano mzuri katika hadithi namba 6 ya “Majivuno ya Kayanda” zilizosimuliwa wilayani Temeke kama ifuatavyo:

> *Hapo zamani za kale katika kijiji cha Keloleli kulikuwa na vijana wawili walioitwa Kayanda na Mugabo walikuwa wafanya biashara wa samaki. Siku moja walisafiri kwa kutumia mashua kutoka*

> *Nyangere kwenda kijiji cha jirani kilichoitwa Nyangoto siku hiyo bahari ilikua tulivu sana. Wakiwa safarini Kayanda alimuuliza Mugabo kwa dharau "Hivi wewe umesoma"?*

Kifungu cha maneno kilichopo hapo juu kinathibitisha kuwa ni kweli wanajamii wamehamasika katika kujiajiri wenyewe katika shughuli ndogondogo za ujasiriamali.

Pamoja na hadithi hio kuonesha wajasiriamali hao na kuonesha kuwa kusoma sio tatizo kwani maisha yanaweza kuendelea na kujisogeza kwa kujiari wewe mwenyewe binafsi na hizo ndoto za serikali ya Tanzania kwa ujumla. Aidha, Shughuli hiyo ya kuuza samaki iliwabidi lazima wapitie katika bahari ni jambo gumu na lenye kuchosha mno. Dhana ya ujasiriamali inajitokeza katika kifungu hicho cha maneno hapo juu kwamba, mjasiriamali ni mpambanaji asiyekata tamaa na hufanya kazi hata katika mazingira magumu.

Kupitia nadharia ya fasihi simulizi, fasihi ina dhima au kazi ya kuelimisha na kufundisha jamii mfano kupitia hadithi namba 6 ya "Majivuno ya Kayanda" inaelimisha na kufundisha jamii kuwa usimdharau mtu usie mjua maana anaweza kufanyika daraja la kukusaidia pia katika kufanya kazi ya ujasiriamali mtu yeyote anaweza kuifanya kazi hii bila kujali elimu yake ilimradi awe na malengo na heshima na kile anachokifanya ili aweze kufikia kile alichotarajia.

Ujumbe tunaoupata katika dhamira hii ni kuwa majivuno si jambo zuri kila binaadamu anafundishwa kutokuwa na majivuno kwa sababu hupelekea dharau, katika maisha huwezi kufahamu mtu atake tokea kukusaidia yawezekana wewe tajiri na mali zako ukahitaji msaada na atakae toa msaada ni maskini ambae hukumtarajia

hivyo basi yatupasha tuishi kwa heshima na adabu katika jamii kwa maana hakuna anaeijua kesho yake itakuaje.

### 4.2.4 Mmomonyoko wa Maadili

Mtunzi anapotunga kazi yake ya sanaa sio jambo ambalo linalotokana na fikra zake au hisia alizonazo tu, bali chochote anachokitungia huwa kinatokana na jamii yake, hali hiyo hutokea kwa jamii kukosekana mwenendo mwema katika jamii zetu. Katika hadithi za watoto wilaya ya Temeke kuhusu jambo hili la mmomonyoko wa maadili ni jambo lililokemewa na wasanii wa hadithi ambazo zinaonesha watoto waliowengi hawaonekani kuwa na furaha wakiambiwa mambo ya msingi na wakubwa zao na mwisho wake huishia kupatwa na matatizo makubwa kutokana na kukana kufuata maadili ya wazazi waokama hadithi namba 5 inavyoelezea katika "Kisa cha Shija"

> *Hapo zamani za kale katika kijiji cha Shamia palitokea kijana mmoja aliyeitwa Shija kijana huyu alikuwa mvivu, mpenda kula na asiyependa shule. Siku moja mama yake Zeituni alimgombeza na kumwambia aende shule ama siangechapwa na kufukuzwa shule, basi kijana alijiandaa akaenda shule alivyofika alikuta wenzake wanafanya usafi wa mazingira, wakamuita "Shiiija" njoo tufagie akakataa",*

Hadithi hii imetuonesha dhamira ya mmomonyoko wa maadili, kwani katika jamii zetu kuna watu wenye kwenda kinyume na maadili ya kutofuata amri na kanuni ambazo zipo katika jamii na kutaka kujitengenezea kanuni zao binafsi na kufanya jambo hilo kuwa na kuyumba kimaisha.

Nadharia ya sosholojia ya fasihi inatupeleka mbali zaidi na kutuonyesha kuwa fanani wa fasihi simulizi wanaujuzi na ustadi katika sanaa husika yaani ubunifu wao ni

mkubwa na wanasaidia kusogeza mbele katika kuielewa fasihi simulizi, kupitia utunzi wa hadithi na usimulizi wake ulivyosimuliwa vyema wilayani Temeke umedhihirisha ni kwa namna gani fanani ametumia ujuzi wa hali ya juu zaidi kutufahamisha mambo yanayojitokeza katika jamii yetu kama vile mmomonyoko wa maadili.

Hivyo kupitia hadithi hii inatupatia ujumbe kuwa kiburi si maungwana mtu mzima au alokupita umri akikuasa jambo basi lisikilize na ulifanyie kazi na vijana waepukane na dharau vijana kama Shija wasijiingize mkumbo mbaya wa kudharau na mwishowe wakapatwa na mtihani. Pamoja na hayo, malezi ya wazazi kwa mtoto ni kumfunda malezi bora, ambayo yatamuwezesha kuishi maisha ya umoja na mshikamano na kuweza kujitambua awe mtoto wa kike au wa kiume na jinsi mabadiliko yanayomkabili ili apambane nayo kimaisha. Sambamba na hilo, nadharia inatupeleka mbali zaidi kwa katika kuona kadri ya mtoto anavyojielewa ndivyo anakuwa msikivu kwa wazazi na hata waliomzunguka.

### 4.2.5 Umoja na Mshikamano

Silaha ya mnyonge ni umoja na mshikamano katika jamii. katika maisha ya kawaida mtu yeyote hawezi kuwa na mafanikio bila kuwa na umojana mshikamano na wenzake ama jamii iliyomzunguka, Katika kijiji cha Kishoju watu waliishi kwa kushirikiana na umoja mkubwa, pamoja na kuishi huko lazima watajitokeza watu ambao hawaeleweki na kuvunja sheria kama inavyotuelekeza katika hadithi namba 1 iitwayo “Tabia ya Nyarushoke,”

> *Paukwa! ... Pakawa! Hapo zamani za kale kulikuwa na kijiji kiitwacho Kishoju. Watu wa kijiji hicho waliishi kwa ushirikiano. Kijiji hicho kiliongozwa na mzee Msemakweli, katika kijiji hicho kulikuwa na kijana aitwae Nyarushoke aliishi na babu yake Alipofika darasa la tano alijiunga na makundi hatarishi."*

Ujumbe tunaoupata katika dhamira hii ni uwepo na umoja na mshikamano katika jamii ni jambo la msingi mno, wanajamii wanatakiwa washirikiane na washikamane katika mambo yote ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Hivyo, kupitia nadharia ya soholojia ushirikiano na mshikamano wa wana jamii ni jambo muhimu kwani bila ya kuwepo umoja huo jamii itaishi katika matatizo makubwa na kutofaulu kabisa.

Pia kwa yule ambae atajitenga na kuwa na peke yake, mambo kadhaa yanaweza kumtokezea na shida hiyo ikawa ni ya peke yake lakini pia kuhudhuria ili kutoa ushiriki wake kwa lengo la kutoa umoja na mshikamano kwenye jamii yake na wezake katika muktadha wowote, shida ya mmoja iwe ni ya wote wanajamii washikamanane na washirikiane katika kulitatua tatizo hilo.

### 4.2.6 Ulevi

Ulevi ni hali ya mtu kunywa pombe au aina nyingine za vileo kama vile madawa ya kulevya, bangi, ugoro, tumbaku na mirungi hata akashindwa kujitambua na kufanya shughuli zake vizuri kama mtu timamu na mwenye nguvu. Katika hali halisi mtu mlevi ni sawasawa na mgonjwa ambaye amelazwa hospitali na kwa hivyo hawezi kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo na kuishia kuwa masikini na tegemezi katika jamii. Kwa mfano, mlevi wa madawa ya kulevya hufika muda dawa zikikolea katika damu ili mtu huyo aweze kuishi vizuri ni lazima apate dawa hizo kila siku

vinginevyo anaweza kupoteza maisha yake (Shapiro na Emde, 1991). Pamoja na kupoteza maisha bado mtu huyo hatoweza kufanya kazi ya aina yoyote ile kutokana na mwili wake kulegea na kukosa nguvu. Kutokana na athari na madhara hayo kuwakatazwa wanajamii wasijiingize katika ulevi kwani ulevi huwafanya kutokuwa na akili na kupelekea kufanya mambo maovu yaliyokatazwa na jamii na taifa kwa ujumla. Kupitia masimulizi ya hadithi za watoto wilaya ya Temeke dhamira ya ulevi na madhara yake imeibuliwa katika jamii kupitia hadithi namba1 ya "Tabia ya Nyarushoke"

> *Wanaolinda kwa bahati mbaya walikamatwa kisha kupelekwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha Walezi wale waliposikia habari hiyo walisikitika sana na kukosa la kufanya, hadithi yangu ikaishia hapo"*

Dondoo hili linabainisha kuwa ulevi ni kitu kibaya sana kwa maendeleo ya mtu mmojammoja na jamii kwa jumla. Mlevi wa dawa za kulevya ni mtu ambaye hata awe na vipaji na ujuzi wa mambo kwa kiasi gani bado ujuzi huo hauwezi kumsaidia kitu katika kujipatia maendeleo binafsi na hata jamii inayomzunguka. Badala yake, mlevi huyo atakuwa tegemezi na mdokozi ambaye atasababisha hali ya umaskini iendelee katika jamii. Ili wanajamii waweze kutumia ujuzi na vipaji walivyopewa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya manufaa yao na jamii yote ni lazima iepuke na kupiga vita matumizi ya vilevya pamoja na ulevi wowote. Hii ni siri kubwa ya kufanikiwa katika maisha inayotolewa na mwandishi kwa jamii au mtu yeyote yule anayetaka kufanikiwa katika maisha.

Katika dondoo hili mwandishi anakiri kuwa wapo baadhi ya watu ambao huingia katika ulevi kutokana na sababu mbalimbali. Jambo la muhimu sana katika njia za

kutibu uathirika wa dawa za kulevya ni mwathirika kukubali kuwa analo tatizo na yuko tayari kukabiliana na tatizo hilo. Mwathirika akijikubali na kuwa pamoja na jamii yake kukubali hali hio basi mtu huyo atarudi katika mstari kama alivyokuwa awali.

Kupitia nadharia ya Sosholojia ya fasihi moja ya dhima ya fasihi ni kukemea maovu yanayofanyika katika jamii kwa mfano kupitia hadithi namba 1 ya "Tabia ya Nyarushoke" hadithi hii inamwelezea kijana aliyekua mtanashati lakini ghafla alitekwa na wimbi la ulevi mpaka akashindwa kuendelea na shule pia inakemea tabia ya ulevi na hanasa ambazo hupelekea vijana wengi kuharibu maisha yao na ndoto walizokuwa nazo zote hupotelea kusikojulikana kwa sababu ya kujiingingiza katika suala la ulevi.

Ujumbe tunaoupata katika hadithi hii ni kuwa ulevi ni adui wa maendeleo katika familia kwani baba anapokuwa mlevi upo uwezekano wa familia yake kukosa mahitaji muhimu ya maisha ya kila siku. Kwa maisha ya siku hizi ambapo pia wapo wanawake ambao ndio wanaofanya kazi ya kuzipatia familia zao mahitaji ya maisha na wao wakiingia katika ulevi husababisha familia zao kukosa mahitaji muhimu kutokana na fedha zote kuishia katika pombe. Hata hivyo, watoto wanapoingia katika unywaji wa pombe basi lazima maangamizi yatatokea katika jamii husika.

### 4.2.7 Uvivu na Uzembe katika Jamii

Kupatikana kwa maendeleo katika jamii ni kitu kinachohitaji utendaji wa kazi kwa makini, kuwajibika, kuachana na uvivu na uzembe katika tasinia yoyote ile ambayo mtu atakuwa anafanya kazi iwe ni ya kuajiriwa au kujiajiri. Waswahili wana msemo kwamba, "Uvivu ni nyumba ya njaa," wakiwa na maana kuwa mtu anapokuwa

mvivu wa kufanya kazi upo wezekano wa mtu huyo kukosa chakula na kuishi maisha ya njaa katika nyumba yake. Uzembe kwa upande mwingine ni hali ya mtu au kikundi cha watu kufanya kazi pasipokuwa na umakini na kusababisha hasara ambayo ingeweza kuzuilika na hivyo kurudisha nyuma maendeleo na kukuza umasikini. Katika jamii ya Watanzania wa leo wapo watu ambao wamekuwa katika hali ya umasikini walionayo kutokana na uvivu na uzembe katika kufanya shughuli za uzalishaji mali. Uvivu na uzembe ni vitu vinavyotokana na utamaduni na malezi ya vile mtu alivyolelewa na wazazi wake. Mfano katika hadithi namba 15 ya "Sizitaki hizi Mbichi,"

> *Hapo zamani za kale kulikuepo mkulima aliyeitwa ... Mkulima alivuna ndizi zote mbivu na mbichi sungura Alipigwa na butwaa akarudi nyumani analia kwa kukosa chakula na hadithi yangu ikaishia hapo."*

Dondoo hili linaonesha ni kwa namna gani uvivu na uzembe unaweza kuungana na kuwa kitu kimoja kuyafanya mazoea hayo ni mabaya na ni ya kudumu na kusababisha hasara kubwa. Hali ya kutegemea kufanyiwa kila kitu na mtu mwingine hufanya ubongo na akili ya mtu huyo anayefanyiwa kila kitu kulala, kudumaa na kutoweza kufikiri juu ya namna mtu huyo anavyoweza kutumia nguvu zake mwenyewe kujipatia kipato cha kuendeshea maisha yake (Comer, 1995). Hali hii husababisha mtu huyo kuwa tegemezi kama vile ambavyo mwandishi amemuonesha sungura ambae aliacha chakula kutoka katika shamba la mzee Gemboi na kuifanya akili yake kuwa, hawezi hata siku moja kufikiri kwamba anatakiwa kujitegemea kwa kupanda chakula chake kikomae ili avune mwenyewe yeye alitegemea Gemboi amfanyie kazi ya kulima yeye aje kuvuna.

Kurejelea nadharia ya Sosholojia ya fasihia mbayo inahitaji kila jamii ichunguzwe peke yake ili kuweza kujua mambo mbalimbali ambayo yanapatikana katika jamii hiyo na kuitofautisha na jamii nyingine zinapochunguzwa kwa wakati tofauti huonyesha utofauti uliopo kati ya jamii moja na nyingine, vivyo hivyo kupitia tasnifu hii ambayo imetafiti hadithi za watoto wilayani Temeke imeweza kutujuza mambo mbalimbali moja ya mambo hayo yanayopatikana katika wilaya hii ni uvivu na uzembe hivyo utafiti huu umetafitiwa katika wilaya ya Temeke pekee na si vinginevyo.

Aidha ujumbe ambao unatolewa na hadithi ya kuwa kila mmoja anapaswa kujitegemea mwenyewe katika maisha na kufanya kazi kwa bidi ili kupata matokeo yaliyo chanya iwe kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumina ikitokea umepeta fursa basi itumie hapo hapo bila kusubiria maana wahenga wanasema ngoja ngoja huumiza matumbo.

## 4.3 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kujadili data na matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu kulingana na malengo mahususi ya utafiti kama yalivyobainishwa katika sura ya kwanza. Sura hii imebainisha hadithi za watoto wilaya ya Temeke, imechambua dhamira zinazojitokeza na nadharia ilivyotumika katika hadithi hizo pamoja na mafunzo yanayojitokeza. Pamoja na hayo zimeweza kujitokeza dhamira kama vile; usafi wa mazingira, wizi katika jamii, ujasiriamali, mmomonyoko wa maadili, umoja na mshikamano, athari za ulevi katika jamii na uvivu.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ya mwisho inahusu muhtasari wa utafiti mzima, matokeo ya tasinifu, utoshelevu wa nadharia ilizotumika katika uchambuzi, uhakiki na mjadala wa data zilizowasilishwa, matokeo ya utafiti, pamoja na mchango wa utafiti. Pia, kuna mapendekezo ya utafiti na hitimisho la utafiti.

## 5.2 Muhutasari wa Utafiti

Tasinifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza imeweka msingi wa kufanyika kwa tasinifu kwa kueleza utangulizi wa jumla, usuli wa tatizo la utafiti na tatizo la utafiti. Pia, malengo mahsusi ya utafiti yameelezwa, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wake. Pia, kuna mpangilio wa tasinifu nzima. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na nadharia zilizotumika katika uchambuzi, uhakiki na mjadala wa data zilizowasilishwa. Sura hii imesaidia kujenga hoja ya kufanyika kwa utafiti huu. Sura ya tatu imeeleza mbinu za utafiti zilizotumiwa katika ukusanyaji, uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa katika taarifa ya utafiti. Sura ya nne ilihusu uwasilishaji na mjadala wa data uliongozwa na nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Masuala mbalimbali kuhusu dhamira za hadithi za watoto katika wilaya ya Temeke yameelezwa katika sura hii. Sura ya tano inahusu muhtasari wa tasinifu, matokeo, mchango wa utafiti uliofanyika, mapendekezo na hitimisho la utafiti.

## 5.3 Utoshelevu wa Nadharia

Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ilitumika katika uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa. Nadharia hiyo ilimwongoza mtafiti kuelezea kwa uwazi katika uchambuzi, uwasilishaji na uhakiki wa data. Hadithi teule zilitazamwa kwa undani namna zilivyochunguza masuala yanayohusu dhamira za hadithi za Watoto katika Wilaya ya Temeke na kuyaweka kama yalivyo na kukubalika kupitia kazi zao. Hadithi teule zilitazamwa moja kwa moja bila chuku ili kufanya uchambuzi na uhakiki wa kina kwa kuzingatia mazingira na wakati ya uandishi wa kazi zinazohusika. Kwa ujumla, nadhari hiyo ilimruhusu mtafiti kupata matokeo kupitia data zilizowasilishwa.

## 5.4 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulihusu, "Kuchunguza Dhamira za Hadithi za Watoto: Mfano kutoka Wilaya ya Temeke". Utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi mawili. Mjadala wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Matokeo ya mjadala wa data za utafiti uliofanyika yameelezwa katika vipengele vifuatavyo:

### 5.4.1 Lengo la Kwanza

Lengo mahsusi la kwanza lilihusu kubainisha dhamira za hadithi za Watoto katika Wilaya ya Temeke. Hadithi ambazo zimesimuliwa watoto katika Wilaya ya Temeke zilionesha dhamira mbali kama vile, usafi wa mazingira, wizi katika jamii, ujasiri amali, mmomonyoko wa maadili, umoja na mshikamano, athari za ulevi katika jamii na uvivu na uzembe. Dhamira zote kwa pamoja zinaonesha namna jamii ilivyo na namna inavyotakiwa kuwa kwa kuzihusianisha na Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi.

### 5.4.2 Lengo la Pili

Lengo mahsusi la pili linahusu kubainisha ujumbe unaopatikana katika hadithi za Watoto katika wilaya ya Temeke. Tasinifu hii imebaini ujumbe mbalimbali kama vile; usafi wa mazingira, tabia ya wizi, majivuno, kupiga vita ulevi, kujitegemea na kufanya kazi kwa bidii

## 5.5 Mapendekezo

Utafiti huu ulihusu kuchunguza dhamira katika hadithi za watoto katika Wilaya ya Temeke. Hivyo mambo yote yaliyojitokeza kwenye utafiti wetu yanatokana na hadithi za watoto kwa jamii husika. Kwa ujumla hadithi za watoto katika tasnifu hii zimechambuliwa kwa kuongozwa na nadharia ya Sosholojia ya Fasihi. Hata hivyo mtafiti ametoa mapendekezo mbalimbali kama ifuatavyo.

### 5.5.1 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine

Mtafiti amependekeza tafiti nyingine zifanyike kwa kuangazia hadithi za watoto wilaya nyingine kutokana na kuhifadhi hadithi zenyewe na kuonyesha jamii kile ambacho kipo ndani ya hadithi husika na tafiti hizo zifanyike kwa malengo tofauti na nadharia tofauti.

### 5.5.2 Mapendekezo kwa Wanajamii

Mtafiti amependekeza wazazi na walezi katika jamii watenge muda kidogo angalau hata kwa wiki mara moja wa kusimulia watoto na vijana wao hadithi wasitegemee tu kusimuliwa hadithi shuleni au kwenye vipindi vya redio na runinga kwamba itatosha kufanya wazielewe vizuri hadithi na kuufahamu umuhimu wake kwa uhalisia vizuri kama ilivyokuwa zamani kabla ya mapinduzi ya sayansi na teknolojia.

## 5.6 Hitimisho

Sura hii imeeleza kwa ufupi mambo yote yaliyojadiliwa katika tasnifu hii. Mambo yaliyotafitiwa na mtafiti wakati wa ukusanyaji wa data uwandani, katika hadithi zenyewe na wakati wa uchanganuzi. Aidha mapendekezo ya utafiti yametolewa ili kuwaongoza watafiti wajao wapate kujua pa kuanzia katika fani hii ya hadithi za watoto. Pamoja na hayo mtafiti anaamini kuwa, tasnifu hii itakuwa chachu ya kuwachangia wanazuoni waliopo na wajao katika kutazamia zaidi utanzu huu wa hadithi ili kuweka bayana hazina iliyomo kwenye fani hii na kufanyiwa utafiti kama zilivyo tanzu nyingine za sanaa jadi. Mtafiti anaamini kuwa tasnifu hii itafunguwa ukurasa mpya na kuweza kuruka vikwazo au kuvunja fikra potofu ya kuwa hadithi za watoto ni upuuzi na mchezo tu. Mtafiti anaamini kuwa tasnifu hii itatoa mwanga mpya na mwelekeo mzuri wa kuithamini na kuipekuwa lulu hii adhimu katika medali ya tanzu za fasihi simulizi.

# MAREJELEO


Ali, J. (2015). "Kutahmini usawiri wa muhusika mwanamke katika hadithi simulizi za Wapemba". Tasnifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Babbie, E. (1992). *The Practice of social research.* 6th Edition. Belmont: Wadsworth Publishers.

Babbie, E. (1999). *The Basics of social research.* Belmont: Wadsworth Publishing Company.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha.* Oxford University Press. Nairobi.

Baxter, L., na Wenzake, (2001). *How to research.* Milton Keynes: Open University Press.

Berg, B. L. (2009). *Qualitative research methods for the social sciences (7 Ed*)". Boston MA: Pearson Education, Inc.

Bernard, H. R. (2000). *Social research methods: Qualitative and quantitative approachies*. Thousand Oaks: Sage Publication, Inc.

Booth, W., et al. (2003). *The craft of research*. Chicago: University of Chicago Press.

Buliba, S. (2014). *Misingi ya nadharia na mbinu za utafiti*. Mwanza: Serengeti Bookshop.

Charkrabarthy, D. (2012). *Research methodology*. New Delhi: Saurabh Publishing House.

Cohen, L. (2000). *Research methods in eduation*. London: Routledge Falmer.

Cooper, R. L. (1989). *Language planning and social change*. Cambridge: Cambridge University Press.

Cryer, P. (2000). *The research student's guide to success*. Milton Keyness: Open University Press.

Doshe, E. A. (2010). "Mchango wa hadithi katika kuendeleza mila na desturi za Waha". Tasinifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Enon, J. C. (1998). *Education research statistics and measurement*. Kampala: Makerere University Press.

Franklin, M. I. (2012). *Understanding research: Coping with the quantitative-qualitative divine.* London and New York: Routledge.

Furlong, N. (2000). *Research methods and statistics: An intergrated approach*. New York: Harcourt Collect Publishers.

Gupta, M., & Gupta, D. (2011). *Research methodology*. New Delhi: PHI Leraning.

Haji, O. M. (2006). *Vipera vya Fasihi Simulizi*. Dar es Salaam: Tanzania Central Printing Services.

Hamad, A. (2008). *Matumizi ya ushairi na muziki wa Kiswahili katika maisha ya kila siku pwani ya Afrika Mashariki*. Zanzibar: BAKIZA.

Israel, M., & Hay, L. (2006). *Research ethics for social scientists.* London: SAGE Publiations.

Kombo, K. D. and Tromp, L. A. D. (2006). *Proposal and thesis writing*: An introduction. Nairobi: Paulines Publishers.

Kothari, C. R. (1990). *Research methodology: Methods and techniques*. New age international (P) limited: New Delhi.

Kothari, C. K. (1993). *Research methodology: Method and techniques*. New age international (P) limited: New Delhi.

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques.* SAGE Publications: New Delhi & Los Angeles.

Kothari C.K. (2008). *Research methodology: Method and technique*. New age international (P) limited: New Delhi.

Leary, M. R. (2001). *Introduction to bebavioral research methods*. London: Allyn Bacon.

Mbarouk, A. A. (1983). *Nyimbo za michezo ya watoto katika fasihi simulizi*. Zanzibar: TAKILUKI.

Mbarouk, S. S. (2011). *Athari za semi za kanga katika jamii.* Tasnifu kwa Ajili ya Shahada ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Merriam, S. B. (1998). *Qualitative research*: *Case Study Application in Education* Revised edition. London: Sage Publications.

Mgogo, Y. P. (2017). "Kuchunguza hadithi za Wanyiha katika kurithisha elimu ya Jadi". Tasnifu ya Uzamivu ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mligo, E. S. (2012). *Jifunze utafiti: Mwongozo kuhusu utafiti na uandishi wa ripoti yenye mantiki*. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGYS).

Msokile, M. (1992). *Misingi ya hadithi fupifupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Mzee, A. (2015). "Kuchunguza maudhui yanayopatikana katika hadithi za watoto katika Jamii ya Wapemba." Tasnifu ya Umahiri wa Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Nyamsende, J. C. (2012). “Usawiri wa taswira za wanyama katika ngano za Waikizu.” Tasnifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Okpewho, I. (1972). *The study of oral literature.* Bloomington and Indian Napolisi: Indiana University Press.

Omar, M. H. (2013). “Nafasi ya hadithi simulizi katika kufunza maadili mema shule za upili visiwani Zanzibar.” Tasnifu ya Umahiri ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Omary, A. S. (2021). “Kuchunguza Vipengele ya Fani jinsi Vinavyoibua Dhamira katika Pwani ya Afrika ya mashariki.” Kongamano la kimataifa la Kiswahili Zanzibar: Bakiza.

Robert, K. (2009). *Case study research: Design and methods.* New York: Library of Congress Cataloging.

Saunders, M. (2007). *Research methods for business students.* (4th ed). London: Prentie Hall.

Sengo, T. S. Y. (2009). *Sengo na Fasihi za Kiinchi*. Dar es Salaam: AERA Kiswahili Research Products.

TAKILUKI, (1981). *Misingi na nadharia ya fasihi*. Sweden: Berlings Arlovs.

TAKILUKI, (1982). *Misingi ya nadharia ya fasihi Zanzibar*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

TAKILUKI, (1983). *Fasihi Simulizi Zanzibar*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

TUKI, (1983). “Utafiti wa Fasihi Simulizi.” Katika makala ya semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili.111: Fasihi Dar es Salaam.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Upagade, V., & Shende, A. (2010). *Research methodology*. New Delhi: S. Chand.

Yin, R. K. (1994). *Case study research*: *Design and methods*. (2nd eds.) London: Thousands of Oaks.

www.gafkosoftcom/swa/hadithi (2009-2014)

Swahili.cri.cn-chapter150301 (7 August 2020)

http://mwalimuwakiswahili.co.tz (17 October2020)

http://www.yoair.com( May 2022)

http://sw.atomiyme.com (May 2022)

http:/sw.m.wikipedia.org./wiki/ (7 Agosti 2020)

http:/sw.m.wikipedia.org./wiki/ (4 Novemba 2023)

Ailyheadlines.com, (13/5/2022).

Sw.warbletoncouncil.org (26 may 2022)

# VIAMBATISHO

## KIAMBATANISHO NAMBA 1. HADITHI ZA PAUKWA PAKAWA WILAYANI TEMEKE

**Masimulizi ya Hadithi.**

**Hadithi namba 1**

**TABIA YA NYARUSHOKE.**

Paukwa!........Pakawa!

Hapo zamani za kale kulikuwa na kijiji kiitwacho Kishoju. Watu wa kijiji hicho waliishi kwa ushirikiano. Kijiji hicho kiliongozwa na mzee Msemakweli. Katika kijiji hicho kulikuwa na kijana aitwae Nyarushoke aliishi na babu yake kwa sababu wazazi wake wote walishafariki.

Nyarushoke alikua kijana mwenye mwenendo mzuri na watu wote wote walimpenda kwa sababu ya tabia njema. Alipofika darasa la tano alianza kujiunga na makundi hatarishi, hivyo alianza kuwa na mwenendo mbaya na alianza unywaji wa pombe, uvutaji wa sigara na wizi. Siku moja yeye na marafiki zake walipanga kwenda kuiba mjini, siku hiyo kulikuwa na askari wanaolinda kwa bahati mbaya walikamatwa kisha kupelekwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha miaka mitano.

Walezi wake waliposikia habari hiyo walisikitika sana na kukosa la kufanya, hivyo yatupasa tuishi kwa mienendo mizuri katika jamii na kuacha tamaa maana tamaa mbele mauti nyuma. Na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 2**

**PANYA NA NYOKA.**

Paukwa!……...Pakawa…..!

Hapo zamani za kale , Panya na Nyoka walikuwa marafiki sana. Siku moja asubuhi Nyoka alitamani nyama tamu sana, Nyoka aliwaza, “Nitapata wapi nyama tamu”? Mara Panya alitokea na Nyoka akajisemea, “Leo nitakula nyama ya Panya”

Panya alinyemelewa na Nyoka, Panya alinyanyuka na kusema, “Vipi rafiki,leo unaninyemelea?” Nyoka alijibu, “Nina hamu ya nyama, tena nyama ya Panya.” Pnya akatoka mbiooooooooo na kutoweka. Urafiki wa Panya na Nyoka ulikomea hapo hapo baada ya kuona nyoka anamuwinda na kummezea mate ili amle nyamaakaona si rafiki ni mnafiki na msaliti. Hadithi yangu ikaishia hapo inatufundisha tuwe makini na marafiki maana wengine ni wasaliti.

**Hadithi namba 3**

**KONDO NA KUKU.**

Hadithi,…….. Hadithi………Hadithi njoo utamu kolea.

Hapo zamani za kale katika kijiji cha Gwata palitokea kijana alieitwa Kondo aliishi huko Bumbwi. Alikuwa na tabia ya wizi na hakutaka kufanya kazi ilia pate ridhiki yake halali bali alitegemea kuiba na kupora vitu vya watu.

Wanakijiji wa Gwata walichoka na tabia yake. Siku moja Kondo aliiba kuku wa jirani yake Chumu maeneo ya Bumbwi, alikamatwa hadi kituo cha polisi na baadae alipelekwa gerezani kwa miezi mine. Huko alifanya kazi ngumu ya kulima, kumwagilia, kufyeka, kujenga na kuchoma tofari. Suruali na shati zake zilimpwaya kwa sababu alikonda mno.

Kondo alikua na upweke, alijuta na kujiiuliza maswali kwa nini aliiba. Alijisemea moyoni, “Njuta, najuta, na sitarudia tena kuiba.

Alipotolewa gerezani kwa msamaha Kondo alibadilika na kuwa kijana mpole na mtiifu hakurudia tena kuiba maana gereza lilimfundisha. Nahadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 4**

**SUNGURA NA FISI.**

Paukwa……..Pakawa……

Hapo zamani za kale walitokea watu wawili watu hao waliitwa Sungura na Fisi. Siku moja Sungura alienda nyumbani kwa Fisi na alikuta kuna nyasi nyingi , Sungura alimuuliza, "Fisi mbona mazingira yako ni machafu sana? Fisi akajibu eeebwana mimi naumwa sana, nasumbuliwa na mgongo kwahivyo siwezi hata kuinama kusafisha mazingira yangu. Bwana Sungura akasema hakuna shaka mimi nitakusaidia kufagia na kuyasafisha mazingira yako. Basi wakati Sungura anainama kuanza kufagia na kuzikusanya taka Fisi aliingia ndani na kuanza kutafuta rungu kwa bahati nzuri aliliona na akalificha kifuani mwake.

Alipofika alimkuta Sungura alishamaliza kufagia na anazoa takataka, hapo hapo Fisi alimpiga rungu la kichwa puuuuuuu!! Hapo hapo Sungura alidondoka chini na kufa halohippo na Fisi akawa ameshajipatia kitoweo cha jioni. Hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 5**

**KISA CHA SHIJA.**

Paukwa……….! Pakawa……..!

Hapo zamani za kale katika kijiji cha Shamia palitokea kijana mmoja aliyeitwa Shija kijana huyu alikua mvivu, mpenda kula na asiyependa shule. Siku moja mama yake Zeituni alimgombeza na kumwambia aende shule ama sivyo angechapwa na kufukuzwa shule, basi kijana alijiandaa na akaenda shule alivyofika shule alikuta wenzake wanafanya usafi wa mazingira, wakamuita "Shiiiiiija" njoo tufagie akakataa, na alivyokataa kufagia walimsemea kwa mwalimu na alichapwa bakora na mwalimu akapewa kazi ya kuokota takataka kwa sababu wenzake walikuwa weshafagia sehemu zote.

Salipomaliza kuzoa takataka wanafunzi wenzake wakamwambia inakubidi unawe mikono kwa sababu umeshika takataka, Shija nae akajibu "Nikanawe wapi na kuna umuhimu gani wa kunawa" ? . Mimi sinawi hata kama kuna maradhi acha tu yanipate nimechoka!

Alikataa kunawa akarudi darasani na wakati wa mapumziko akachukua chakula na kula bila kunawa mikono. Baaada ya muda mfupi tu Shamia alishikwa na tumbo la kuhara, yaani kwa muda mfupi ambao alianza kuhara alikua amechoka hoi bin taaban. Alipewa huduma ya kwanza yalikuwa ni maji ya moto yenye chumvi na sukari, baadae alipopata nafuu Shija alirejea nyumbani na kumwambia mama yake yaliyomkuta alivyokuwa shule. Toka siku hiyo Shija aliacha dharauna kuanza usafi kwa kuzingatia kanuni za afya na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 6**

**MAJIVUNO YA KAYANDA.**

Hadithi…….Hadithi…….Hadithi njoo ukweli njoo utamu kolea!

Hapo zamani za kale katika kijiji cha Keloleli kulikuwa kuna vijana wawili walioitwa Kayanda na Mugabo walikuwa ni wafanya biashara wa samaki. Siku moja walisafiri kwa kutumia mashua kutoka Nyangere kwenda kijiji cha jirani kilichoitwa Nyangoto siku hiyo bahari ilikua tulivu sana. Wakiwa safarini Kayanda alimuuliza Mugabo kwa dharau "Hivi wewe umesoma" Mugabo alijibu; "Hapana sijasoma". Je, wewe unajua kuogelea?Kayanda akajibu; "Nimesomea sheria, sasa kuogelea kutanisaidia nini?

Punde si punde wakiendelea na mazungumzo ya hapa na pale mara upepo mkali ukavuma na kupelekea bahari kuchafuka hapo hapo mashua ilianza kupoteza uelekeo na kuanza kuzama polepole. Mugabo alimuonea huruma Kayanda kwa jinsi alivyotapatapa na akaamua kumuokoa. Kayanda na Mugabo wakawa marafiki na toka siku hiyo, Kayanda alithamini utu na kuacha majivunona Mugabo akatamani kusoma na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 7**

**MAMA NZI NA KIPEPEO.**

Paukwa………!Pakawa………!

Hapo zamani za kale kulikuwa na marafiki wawili wa kwana alikuwa ni Kipepeo na wa pili ni Nzi. Walikuwa na maeneo yao ya kutawala rafiki Nzi alipenda kutawala sehemu chafu, na Kipepeo alipenda kutawala maeneo safi na yenye maua na mazingira mazuri, siku moja Kipepeo alimuuliza Nzi ; “Rafiki yangu mbona unapenda kutawala sehemu chafu?” nae Nzi akajibu achana na maisha yangu.

Baada ya wiki moja Nzi aliugua kipindupindu na akashindwa hata kuruka ili apae. Watoto wake walimuuliza mama unaugua ugonjwa gani? Nae akawajibu wanangu nilikua na mazoea ya kutawala sehemu chafu rafiki yangu Kipepeo alinikataza lakini nilimdharau na hivi ndivyo nilivyopata ugonjwa huu mbaya wa kipindupindu. Watoto wa nzi walimuuguza mama yao hadi umauti ukamkuta na akafariki dunia. Hadithi yangu ikaishia hapo na inatufundisha tusipende tusipendekukaakatika mazingira machafu ni hatari kwa afya zetu.

**Hadithi namba 8**

**WATOTO WATATU.**

Paukwa……..!Pakawa……..!

Hapo zamani za kale kulitokea watoto watatu watoto hao waliitwa Tabu, Bera na Mwahija ni wanafunzi wa darasa la tano katika shule ya mazoezi ya Motogoro iliyopo huko Songambele. Siku moja Tabu aliamka mapema alfajiri kama ilivyokua kawaida yake na kuwapitia marafiki zake Bera na Mwahija, njiani walikutana na mzee Mapunda ambapo Tabu alimsalimia lakini rafiki zake hawakumsalimia.

Mzee Mapunda akauliza; "Nyie wajukuu mbona hamnisalimii" Bera na Mwahija walinyamaza kimya hawakusema kitu na mzee Mapunda aliwaasa wasifanye hivyo maana hiyo si tabia njema ni ukaidi, au mnataka tuongozane wote hadi kwa mwalimu wenu wa nidhamu nikamweleze tabia zenu mbaya ili muadhibiwe?

Bera na Mwahija wakasema; "Tafadhali mzee tunaomba utusamehe na hatutarudia tabia hii na tutakua watoto wema wanao salimia kila mtu". Hatimaye tabuakawakumbusha utekelezaji wa ule wimbo waliokuwa wakiimba kipindi wapo darasa la I na la IIna unaimbwa hivi;

*" Tuamkapo asubuhi tuwasalimu wazazi*
*Tuwasalimu wazazi,*
*Shikamo baba shikamoo mama*
*Hiyo ndo tabia njema"*

Hadithi yangu ikaishia hapo, hadithi hii inatufundisha tuwe na tabia njema.

**Hadithi namba 9**

**KISA CHA WATOTO MAPACHA.**

Paukwa………!Pakawa…….!

Hapo zamani za kale palikuwepo na watoto mapacha mmoja aliitwa Hissa na mwingine Mussa. Hissa alikuwa ni mtoto mwenye tabia mbaya na mdokozi na Mussa alikuwa ni mtoto mzuri, mpole na mtaratibu. Siku moja mama yake alimtuma akamnunulie unga dukani nae Hissa akaitikia haya mama nitakwenda nipatie hiyo hela ili niwahi kurudi , mama yake alimpatia pesa kumbe kimoyo moyo anafikiria kua hatorudisha ile pesa. Nyumbani mama aliunga mboga ikaiva na mama yake aliinjika chungu cha ugali ili asonge ugali.

Mama yake alisubiria mpaka akachoka ikabidi amtume Mussa akamtafute mdogo wake, Mussa alikwenda dukani hakumkuta ikambidi atembee njiani kumtafuta mdogo wake alitafuta mpaka akachooooka na akaamua kurudi nyumbani saa moja usiku.

Mama yake alivyomuona Mussa amerudi akamuuliza Hissa yuko wapi nae akajibu mama nmemtafuta lakini hajapatikana kusikia hivyo mama yake alistuka sana akakaa chini na kuanza kulia mpaka leo hii Hissa hajaonekana na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 10**

**SUNGURA NA FISI.**

Hadithi hadithi………..

Hapo zamani za kale kulikuwepo na Sungura na Fisi, siku moja Sungura alikua na shida ya upanga na sungura alikua na shida ya sukari. Fisi akafikiria hivi upanga nitaupata wapi? Hivyo akaamua kwenda kwa rafiki yake Sungura, alipofika nyumbani kwa rafiki yake alimkuta Sungura amekaa anawaza sukari ataipata wapi? Akaamua kumuuliza rafiki yangu unawaza nini nae Sungura akamjibu; rafiki yangu natafuta sukari nitaipata wapi?

Heeeeee! Yaani rafiki yangu unataka sukari tu unawaza? Sasa mimi ntakupatia sukari lakini na mimi  nina shida ya upanga Sungura akajibu heeee! Upanga mimi nitakutengenezea usipate shida. Wakaondoka na kuagana kwa ahadi ya kesho wangeonana na kutimiziana ahadi zao. Kesho ilipofika Sungura akachukua kipande cha mti akakichonga kama panga na akakipaka rangi inayofanana na panga, Fisi nae akachukua gunia akalijaza mchna kwa juu akanyunyuzia sukari kidogo walipoonana walipeana vitu. Kila mtu alienda kwake akijisifu amemkomoa mwenzake kumbe wamekomoana na Sungura alipofika nyumbani kufungua kiroba chake akakakutana na mchanga na Fisi kwenda kukata mti panga likavunjika kumbe lilikua ni mti tu. Hadithi hii inatufundisha tuwe wakweli na wawazi na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 11**

**KIDOLE KIMOJA HAKIVUNJI CHAWA.**

Paukwa…..!..........Pakawa………...!

Hapo zamani zakale palikuwa na kijiji kimoja kilichoitwa Ushirikiano, wanakijiji wa ushirikiano walikuwa na mazoea ya kufanya kazi kwa pamoja. Hapo kijijini kulikuwa na mzee aliyeitwa Chakasi mzee huyo alikuwa ni mwenye hekima na busara na watu walimwamini kwa mchango wake wa kuendeleza kijiji hicho mbele zaidi.

Siku moja mzee Chakasi akiwa manaelekea shambani kabla ya kufika maeneo ya shamba alisimama jirani na mti ulioitwa Mokka mti huo ulikuwa mbele yake na akaanza kulitazama shamba kwa mbali. Ghafla bin vu! Akamuona simba dume pembezoni mwa shamba lake, hapo hapo mzee yule aligeuza uelekeo na kurudi nyumbani na huko alikwenda kutoa taarifa kwa Mfalme ya kuwa tumevamiwa na simba hivyo tujipange.

Wanakijiji walishirikiana kumzunguka simba mpaka wakamuweka kwenye mtego na walifanikiwa kumuua simba huyo. Watu wote walifurahi sana na walipongezana kwa ushirikiano huo toka siku hiyo kila jambo likifanywa kwenye kijiji hicho ni lazima wote washirikiane ili kuleta maendeleo kijijini hapo, hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 12**

**KISA CHA MPENDA KULA NA NDUGUZE.**

Paukwa……!...........!Pakawa……….!

Hapo zamani za kale palitokea kijana mmoja aliyeitwa Mpendakula. Siku moja Mpendakula alikwenda sokoni kununua samaki, viungo na mchele. Baada ya hapo alikwenda kununua soda, alivyomaliza kununua alirudi nyumbani. Alianza kupika na alivyomaliza akaamua aende kwenye shughuli zake ndogo ndogo zinazomuingizia kipato.

Majira ya saa kumi na mbili jioni alianza kupakua chakula na akaanza kula mara akasikia mlango unagongwa akakimbilia chumbani na kuficha chakula kabatini na akarudi kufungua, ile kufungua tu akakutana na ndugu zake.

Aliwakaribisha na wakashukuru lakini walimtaarifu kuwa wamechoka na wananjaa sana, yeye aliwajibu kuwachakula kimeisha kwa sababu walikuja bile taarifa hivyo alipika cha kumtosha yeye tu, hivyo wageni walienda kuoga na walielekea moja kwa moja kulala. Mpendakula aliingia chumbani na kula chakula kwa bahati mbaya mwiba ulimkaba akaanza kuhangaika akajaribu kuingiza vidole kooni labda mwiba ungetoka lakini haikuwezekana aliendelea kuumia, alivumilia kwa muda lakini maumivu yalimzidi na akashindwa kuvumilia akaanza kupiga kelele Mama! Mama! Mama! Mama! Mama! Nakufa mimi

Wageni walistuka sana ikabidi waingie wakatoe msaada wa haraka kwa Mpenda kula maana alizidisha kelele walivyomuona alikuwa ni mtu aliyekuwa anakula chakula na

alikuwa amekabwa na mwiba hivyo ndugu yake alikunja tonge la ubwabwa na kumpa ameze baada ya kumeza punde si punde mwiba ulitoka. Basi kwa aibu Mpendakula aliona aibu sana na aliinama chini kwa aibu na akawaomba nduguze msamaha kwa kilichotokea. Hadithi yangu ikaishia hapo na inatufundisha tuache uchoyo na roho mbaya.

**Hadithi namba 13**

**NTIGA NA WENZAKE.**

Paukwa…..! Pakawa…….!

Hapo zamani za kale katika kijiji cha Kwilo palitokea kijana mmoja wa makamo aliyeitwa Ntiga alisoma shule ya msingi Mkwajuni na baadae likuta shule na kujiunga na vijana wahuni waliokuwa na tabia ya kukaa na kuvuta bangi na kuishoinda dampo wakiocheza kamali na ikifika mida ya jioni na wanakaa uchochoroni na kukaba watembea kwa miguu.

Siku ya ijumaa jioni kama ilivyokawaida yao walikaa kijiweni na kuanza kupanga kesho itakuwaje na watakwenda duka gani kuifanya kazi yao ya uvamizi ili kujipatia faida? Walipanga waende dukani kwa Mpemba maana kila siku wanapanga lakini inashindikana, wakiendelea kujadili hawakujua kama kuna mtu anawasikiliza hivyo walipanga mpaka muda wa kufika ili waianze kazi yao na waliagana na kuondoka nae msamalia mwema aliende kutoa taarifa kituo cha polisi cha karibu na akaondoka.

Ilivyofika muda waa saa nane usiku kama ilivyopangwa Ntiga na wenzake walianza kuwasili eneo la tukio na pasi na kuchelewa walianza kuifanya kazi waliyoipanga

toka juzi mchana na wakati huo askari walikua wameshafika muda mrefu na wamejificha wanawatizama wanavyowasili. Basi ile wanaanza kugonga nyundo ukutani puuuuuu! Askari nao walirusha risasi hewani na walitarajia vijana hawa waharifu wangekimbia lakini waliendelea kupambaa na askari katika mabishano hayo wawili walifariki na wawili walikamatwa na polisi.

Hadithi hii inatufundisha tusiwe na tamaa katika maisha na wizi ni mbaya sana na hadithi hii ikaishia hapo.

**Hadithi namba 14**

**CHURA NA PANYA.**

Hadithi…… Hadithi……..Hadithi………!

Hapo zamani za kale walikuepo Chura na Panya wanyama hawa walikuwa marafiki sana, siku moja Chura alipatwa na wivu mkubwa kwa kumuona rafiki yake Panya anang’aa na ni mwenye manyoya ya kutereza kama sufi, tena akamuuliza rafiki yangu unafanya ninni hadi unang’aa na ngozi ya kutereza namna hii.

Panya kwa upendo akamjibu, kwanza mimi kila siku naoga maji yenye umoto ambayo nmechemsha lakini kabla Panya hajamaliza Chura akadakia na akamuuliza unaruka na kuingia humo ama?

Panya akamjibu hapana huingii, Panya akaendelea ukisha yachemsha, lakini pia kabla hajasema Chura akadakia tena unaruka unaingia tena humo? Panya kwa hasira akasema heee! Hebu nipishe mbona huna subira huku Panya akiondoka.

Basi Chura kwa kujisifia akasema nmeshakuelewa kumbe hukutaka nijue kwa nini una ngozi kama sufi ili nisikupite unanionea wivu na hivi unajua najua kuruka ruka mbona nitakupita uzuri?

Basi chura akaondoka akaenda kwake, Kruuu! Kruuu! Kruuu! Alipofika nyumbani akachemsha maji alipohakikisha kabisa akaruka vizuri Chubwi! Kwenye maji ya moto na kutua humo hapo hapo alipatwa na vidonda mwili mzima na ngozi yake ikawa yenye mabakamabaka na hadithi hii ikaishia hapo.

**Hadithi namba 15**

**SIZITAKI HIZI MBICHI.**

Hapo zamani za kale kulikuwepo na mkulima aliyeitwa Gemboi aliishi kijiji cha Mwendapole alikuwa analima nafaka na mazao mengine kama migomba, minazi na matunda mengine kama embe, fenesi na machungwa.

Siku moja sungura na rafiki zake walipita shambani mwa mkulima Gemboi na kukuta ndizi zimeiva shambani humo rafiki zake Komba wakamwambia Sungura ndizi hizozimeiva ungechuma zitakusaidia ukifika nyumbani, Sungura akajibu alaaa! Mimi sizitaki hizo mbichi mpaka ziive ndo nile. Wakaondoka hadi nyumbani walipofika Komba alichuma madafu ya nazi ili apate pombe, akanywa akarudi nyumbani Sungura alivyoona Komba kaondoka akaamua na yeye azaende kufuata zile ndizi alizoacha shambani mwa Gemboi, alipofika alikuta mwenye shamba kachuma ndizi zoote mbivu na mbichi sungura alipigwa butwaa na akarudi nyumbani analia kwa kukosa chakula na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 16**

**TEMBO NA FISI.**

Paukwa….., Pakawa……!

Hapo zamani za kale alikuwepo Tembo, Tembo alikuwa ndiye mfalme, wanyama wote walimuheshimu na kumwabudu, katika kijiji chao kulikuwa na shida kubwa ya chakula ili kutatua tatizo hilo, Tembo aliona ni nafuu awaamrishe wananchi wakee walime chakula cha kutosha ili kuondokana na tatizo. Wanyama wote walikubali isipokuwa Fisi akakataa akasema mimi nitalima peke yangu sihitaji kuungana na wengine.

Wanyama walilima na Tembo wakapata chakula kingi sana na Fisi hakuweza kulima peke yake kilichobaki ikambidi akaibe chakula kwenye shamba la ushirika wakati wa usiku, walipomuona walimkamata Fisi na alipigwa mno mpaka akasema ameahidi kuacha wizi. Hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 17**

**HADITHI YA MKE MWENZA.**

Paukwa…….Pakawa…….!

Hapo zamani za kale alikuwepo bwana Mtera na mke wake walikuwa na watoto wawili waliishi katika mtaa wa Mbotoni. Mtera alikuwa ni mkulima wa mazao ya biashara na mkewe alikuwa ni mama wa nyumbani.

Ilikuwa ni kawaida ya Mbotoni kulima mazao mengi lakini hakupata kuvuna mengi zaidi lakini mwaka uliofuata alilima na akapata mazao mengi sana na hapo hapo

Mtera alibadirika na kuanza fanya vituko kwa kumpiga mpaka kumuumiza, kumtukana mkewe kwa sababu alipata pesa nyingi mno baada ya kuuza nafaka.

Aliendelea na tabia ya kumpiga mkewe mpaka alivyo oa mke wa pili akaendekeza na hanasa katika jamii yake.

Maisha yaliendelea kua magumu kwa mkewe maana mke mdogo alikuwa anamchongea maneno kwa mumewe ili apigwe na siku moja alisema mke mwenzie hakwenda shamba na alipika chakula kibichi. Mtera alimpiga sana mkewe mkubwa mpaka akafariki dunia.

Siku ya maziko mke mdogo akaanza kujiliza kinafiki huku anaongea;

*"Ndi….,ndi……ndi…..*
*Mke mwenzangu lala salama…!*
*Ndi……ndi ……ndi……"*

Marehemu akamjibu mke mwenzie hivi;

*"Si wewe hapo!x2*

*Kunichonganisha kwa mume wangu…*

*Ndi …….ndi……ndi…*

Hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 18**

**LIKONOKA NA MAISHA.**

Hadithi……Hadithi……..

Hadithi njoo………Utamu kolea……..

Hapo zamani za kale alikuwepo kijana Likonoka na mwenzake Maisha hawa walikuwa na maisha magumu na yenye taabu sana waliishi jirani na shule ya msingi Nyakita walitumia fursa hiyo kuuza chakula na bidhaa ndogondogo hapo shuleni.

Siku moja Likonoka akamuuliza mwenzake; hivi Misha rafiki yangu haya maisha na hali ngumu hivi tutaviishi hadi lini?

Maisha akajibu; hapana rafiki yangu mimi binafsi siyapendi maisha haya na ndiyo maana tunapambana ili tuweze kutoka kwenye ugumu huu wa maisha.

Likonoka akaongezea;sasa inabidi tutoke tukatafute mali na maisha mazuri. Waliondoka asubuhi na mapema walitembea sana walifika huko usiku sana katika kutembea walifika kwenye mti mnene na wakakutana na babu anawaulizia;

**Babu:** wajukuu zangu hamjambo na mnatafuta nini?

**Likonoka na maisha:**hatujambo babu shikamoo, maisha, maisha tunatafuta tuna shida mno!

**Babu:** mtaweza mitihani nyie?

**Wote:**tutaweza tu babu.

**Babu:** haya lambeni ngozi yangu kuanzia miguuni mpaka makamasi na tongotongo mpaka kichwani.

Walifanya hivyo na walivyomaliza yule babu aliwapa mzigo mzitouliofungwa kwa ngozi ya ng'ombe walibebe na kurudi nyumbani, walivyofika nyumbani walikuta mzigo ule ulifungwa umewekewa vipande vya dhahabu waliuza na wakapata pesa na maisha mazuri na wakajiendeleza kwa biashara na mifugo. Hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 19**

**BI NYAU.**

Paukwa……!Pakawa……!

Hapo zamani za kale, alikuwepo Bi Nyau alikuwa anafuga mifugo mbali mbali na wanyama kama Mbwa , Tumbili na Punda.

Mbwa wake alikuwa ni mzuri sana alikuwa msikivu na mkali pale inapobidi alikuwa anafungiwa ndani na kufunguliwa usiku wa saa tatu (3) kila mtu alimtamani mbwa yule kwa jinsi alivyokuwa mzuri.

Siku moja Bi Nyau alikwenda kwa dadaake Mlimauni kumsalimia alivyomaliza kumsalimu alirejea nyumbani kwake, alivyofika hakupokelewa na mbwa wake Tabia kama alivyozoea ilibidi azunguke nyuma ya nyumba yake lakini hakumuona mbwa wake ikabidi aanze kuita;….Tabia,…Tabia….Tabia…..lakini mbwa hakuitika mwisho wa siku akaanza kuimba.

*"We Tabia mpendwa……Tabiax2*
*Uwapi mpendwa……………..x2*

Kwa bahati nzuri mbwa wake nae akamjibu hivi;

*"Mie …….Tabia……mie Tabia…*
*Mlezi wangu nihuku mpendwa…*
*Natupwa baharini mpendwa mpendwa*
*Navunjwa miguu mpendwa, sababu ni wivu mpendwa…….*
*Nifate mpendwa………………..."*

Bi Nyau alikwenda baharini na akamkuta mbwa wake kavunjwa miguu alimchukua na kwenda kumkanda miguu kwa kutumia maji yamoto yenye chumvi mpaka akapona, tokea siku hiyo Bi Nyau akitoka na kwenda sehemu yoyote ni lazima aondoke na mbwa wake. Hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 20**

**CHUMBA CHA 3.**

Paukwa……! Pakawa…..!

Hapo zamani za kale kulikuwepo na mtu na mkewe, mume aliitwa Kehanga na mkewe aliitwa Maua. Walijenga nyumba yao yenye vyumba 6 na walikuwa na uwezo wa mali na fedha na walijaaliwa kupata watoto watano (5) na walianzishwa shule wakawa na maendeleo mazuri sana shuleni.

Katika nyumba hiyo ya bwana Kehanga yenye vyumba6 alimuonya mkewe asiingie chumba cha tatu katikati na kisifanyiwe usafi wala kisifunguliwe lakini vingine vyote aliruhusiwa kuingia.

Siku moja mida ya mchana mkewe alisikia kama kuna kitu kinafurukuta kwa fujo sana kwa kuugonga mlango na ukuta kwa kasi ya ajabu. Mama alibaki amehamaki

asijue cha kufanya akabaki asnasema; “Ama kweli siku ya kufa nyani miti yote hutereza” alisema hivyo kumaanisha mtu unapata tatizo siku ambayo hakuna mtu wa kukusaidia. Siku hiyo watoto wake wanaosoma walikwenda shule nyumbani alibakia na mtoto wa miezisita (6).

Wakati gozo hilo likiendelea katika chumba cha 3 katikati, mke wa Kehanga alikua anajiandaa kukimbia na mtoto wake mdogo mara ghafla huku nyuma mlango ulifunguka na joka kubwa lilitoka kumbe mumewe alisasahau kufunga mlango na funguo wakati wa usiku alipokuwa anakagua. Joka lilitoka kwa ghadhabu na likammeza mtoto palepale kuona vile mama yake alikimbia sana nakupiga yowe kwa majirani kusudi asaidiwe, majirani walifika na walimkuta nyoka hana nguvu za kukimbia kwa sababu alimmeza mtoto alipigwa palepale na akafa.

Kehanga alivyorudi nyumbani jioni alipata taaarifa hizo na alisikitika sana kwa kilichompata naakasema ama kweli tamaa mbele mauti nyuma nilipatwa na tamaa ya mali mwisho wake nmempoteza mwanangu.hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 21**

**KONDO MTOTO WA CHIWA.**

Hadithi…..Hadithi………Hadithi njoo Utamu Kolea!

Hapo zamani za kale Chiwa na mke wake Kasuku. Chiwa alikuwa ni mvuvi na walijaaliwa kupata mtoto mmoja aliyeitwa Kondo na mkewe alifariki muda mfupi

baada ya kujifungua inasemekana kondo la nyuma lilikataa kutoka na ndio maana mwanae aliitwa Kondo.

Kondo alikuwa mtoto mwema na mwerevu sana na alilelewa na bibi yake mzaa mama na baba yake alimchukua alivyofikisha umri wa miaka mitatu (3) ili aende kuanza shule, wakati akisoma alikuwa mwenye bidi na shule na siku zote alikuwa mtoto mzuri kwa wazazi na shuleni pia. Siku moja baba yake alikwenda pwani kuvua samaki, huku nyumbani Kondo alikuwa amesharudi kutoka shule na anajiandaa kupika chakula jikoni.

Wakati anaandaa mafiga jikoni na kutoa jivu ndipo alipogundua amegusa kitu chenye joto na kinatereza, kuchunguza kwa makini alikuwa ni nyoka aina ya koboko alichofnya Kondo hakustuka alisimama kiujasiri na kutafuta fimbo nene alisimama jirani na jiko yao maeneo ya mlangoni alihakikisha anapiga mara mbili tu na nyokka tayari ameshakufa.

Baada ya zoezi hilo aliita majirani wakaja na baba yake alikuwa amerudi kutoka pwani akajionea tukio hilo na kijijini kote walimtawaza na kumchagua kuwa chifu katika kijiji chao, licha ya umri wake mdogo lakini Kondo aliongoza vizuri sana na sifa zake zilitangazika mpaka kijiji cha jirani, na hadithi yangu ikaishia hapo.

**Hadithi namba 22**

**BINTI CHAUPELE.**

Paukwa……..!Pakawa………!

Hapo zamani za kale alikuwepo binti mzuri wa sura na umbo aliishi kijiji cha Songambele, alikuwa mrefu wa wastani shingo ya upanga na macho ya golori yaliyobebelewa na ngozi ya hudhurungi na alibahatika kusoma shule ya upili Songambele. Baada ya masomo alibahatika kufaulu lakini hakubatika kuendelea na masomo kwa sababu wazazi hawakuwa na uwezo wa kumuendeleza kimasomo hivyo alisalia nyumbani kusaidia kazi ndogondo.

Akiwa nyumbani walitokea wachumba rukuki karibia ishirini lakini wote hakuwataka kwa sababu hawakuwa na vigezo alivyovitaka yeye, wengi hawakuwa na sura nzuri na walikuwa hawajui kusoma.

Miezi sita ilipita akatokea mchumba mwingine mzuri wa sura na mwenye pesa za kutosha yeye kubadirisha mboga. Chaupele akasema bahati yangu ipo hapahapa na huyu ndio chaguo langu nilosubiri kwa muda mrefu wazazi pokeeni mahari upesi pasi na kuchelewa.

Mali ilipokelewa na harusi ikafanyika ya kifahari watu walikula na kusaza na binti Chaupele aliondoka kwenda kwa mumewe, lakini kufika tu siku ya pili yake akaanza kuona mambo ambayo hayaelewi kwa sababu mumewe alikuwa na mkia mrefu sana kama samaki taa na nywele zake mpaka mgongoni siku ziliposonga mbele Chaupele aligundua kua yule bwana ni zimwi alipiga kelele na akakimbia kurudi nyumbani kwao ile anafika tu alianguka chini na akazimia kwa muda wa siku 7 na hadithi yangu ikaishia hapo.

## KIAMBATANISHONA: 2

### Kiambatanisho namba 2.1 Ushuhudiaji

**Utangulizi ,**

Ushuhudiaji ni njia mojawapo ya mbinu katika ukusanyaji wa data ambayo mtafiti atatumia katika utafiti huu. Njia hii mtafiti atakwenda katika eneo husika na kushuhudia kile atakachokitafiti (Mulokozi, 2010). Mbinu hii itamuwezesha mtafiti katika kufanikisha ukusanyaji wa data za utafiti na itafanyika kama ifuatavyo.

Kitakachoshuhudiwa:

Mtafiti atafika eneo la tukio ambalo atafanyia utafiti huo na ataanza kwa kusalimia wenyeji wake ambao atawakuta katika eneo hilo, baada ya salamu atajitambulisha na kueleza lengo kuu lililofanya afike mahali hapo ambalo ni kufanya utafiti wa kuchunguza dhamira katika hadithi za watoto Wilayani Temeke.

Ataandaa vifaa ambavyo atatumia kufanyia utafiti huo kama vile peni, karatasi, kitabu, kamera, tepurekoda na vinginevyo ili kukusanya data ipasavyo.

Pasipo kuchelewa mtafiti ataanza kuiuliza hadhira yake au watafitiwa ambao amekutana nao kuhusu maana ya neno hadithi wanaweza kuwa watoto au vijana au wazee ambao wameambatana na watoto hao (watoto / wanafunzi waliotumiwa katika utafiti huu ni kuanzia darasa la 4 mpaka la 7.

Baada ya kusikiliza maoni hayo kuhusu maana ya hadithi mtafiti nae anaweza kuongezea maarifa kwa kutoa maana kamili ya neno hadithi ili kuongeza uelewa wa dhana hiyo.

Mtafiti atauliza hadithi ambazo watoto wanahadithiana Wilayani Temeke na dhamira gani zinatokana na hadithi hizi?.

Mtafiti atauliza ni ujumbe gani unapatikana katika hadithi za watoto Wilayani Temeke?

Mtafiti ataomba asimuliwe hadithi za paukwa pakawa na watoto watatu ambao watakuwepo katika eneo au mazingira hayo ambamo utafiti unafanyikia na wataanza kwa kusema hivi;

*Mtoto wa1, Paukwa……..*

*Mtafiti na wengine Pakawa …….*

Mtafiti atasikiliza hadithi hizo atatoa shukrani kwa kusimuliwa hadithi na atauliza hadithi hizo zinatoa funzo au ujumbe gani kwa jamii.

Baada ya usikilizaji wa hadithi hizo mtafiti ataendelea na utafiti wake kama ambavyo alikua amepanga ratiba yake na atakua ameshuhudia vyema kabisa.

Mtafiti ataishukuru hadhira na jamii kwa ujumla kwa kumpa mashirikiano mazuri , mpaka akamaliza zoezi la usikilizaji wa hadithi na ukusanyaji wa data vizuri zilizo tolewa na kusimuliwa kwa utulivu na atawaaga na kuondoka.

**Kiambatanisho namba 2.2 Dodoso/ Usaili**

**Utangulizi,**

Dodoso ni njia ya ukusanyaji wa data ambayo mtafitiwa ndiye hujaza majibu kulingana na utafiti unavyohitajika (Kothari 2004). Dodoso inatokana na neno dodosa ambalo lina maana ya kudadisi mtu kwa kumuuliza maswali (TUKI, 2004).

Kitakachosailiwa/kudodoswa;

Katika utafiti huu, mtafiti atatumia dodoso kwa watoto na watu mbali mbali ambao wanazisikiliza na kuwafundisha watoto hadithi hizo ili kupata ujumbe, funzo, dhamira kutoka kenye hadithi za watoto.

Yafuatayo ni maswali yatakayo ulizwa na mtafiti wakati wa kukusanya data.

Je nini maana ya neno hadithi?

Ni hadithi zipi wanazohadithiana watoto Wilayani Temeke?

Ni dhamira zipi zinazotokana na hadithi za watoto

Ni ujumbe gani unaopatikana katika hadithi za watoto?

Katika wilaya hii hadithi hizi zinaendelezwaje ili zisipotee hasa katika kipindi hiki cha sayansi na teknolojia?

Je watoto Wilayani Temeke wanatambiana hadithi wenyewe kwa wenyewe?

Watoto Wilaya hii ya Temeke wanapata nafasi ya kusimuliwa hadithi za kijadi za paukwa….pakawa?

Je naweza kupata watoto watatu ambao wanaweza kunisimulia hadithi za paukwa….pakawa?

Hadithiza watoto Wilayani Temeke zina nafasi gani katika kufunza watoto?

Je hapo zamani hadithi za watoto hapa Wilayani Temeke zilikuwa zinatambwa wakati gani?

Kwanini zilikuwa zinatambwa wakati huo?

Je kuna athari yoyote ingetokea endapo mtu angeitamba muda wowote apendao yeye na si muda uliopangwa?

Mtafiti ataishukuru hadhira waliomsaidia wakati wote wa kazi kwa mashirikiano mazuri waliompatia mpaka kufikia kikomo na atawaaga na kuondoka.

**Kiambatanisho namba 2.3 Mbinu za kuchambua data.**

**Utangulizi**

Uchambuzi wa data ni kitendo cha kutolea ufafanuzi data zitakazokusanywa kwa namna ambayo itasaidia kujibu maswali ya utafiti na kutimiza malengo ya utafiti. Data za utafiti zitachambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo.

Mbinu zitakazotumika

Mtafiti atatoa data zake kwa maelezo mbinu hii ni muhimu kwa mtafiti kwa sababu itamuongoza kuchambua na kufafanua kwa uwazi data ambazo zitakusanywa na kuzifanyia utafiti Zaidi Data zitachambuliwa kwa kuzingatia dhamira zitakazopatikana katika hadithi za watoto wilayani Temeke.

Uchambuzi wa data utafata hatua mbalimbali kama zifuatazo; kwanza kuzisoma hadithi zote na kuziainisha, pili kuchambua dhamira katika hadithi wanazotamba au kutambiwa watoto pamoja na ujumbe unaopatikana katika hadithi hizo.

Mtafiti atatoa hitimisho kuwa atachambua data kwa kuzingatia vipengele vitatu ambavyo ni dhamira zitakazopatikana katika hadithi za watoto wilayani Temeke, ujumbe utakaopatikana katika hadithi za watoto wilayani Temeke na kuziainisha hadithi hizo za watoto wilayani Temeke.

**Kiambatanisho namba 2.4 Usanifu wa Utafiti.**

**Utangulizi**

Usanifu wa utafiti ni muongozo uaoelezea namna utafifi utakavyofanywa, utafiti huo utakua ni wa namna gani na data zitakusanywa kwa kutumia mbinu gani?

Haya ni maelezo yanayotolewa kuelezea muundo au umbo la utafiti husika tangu katika kukusanya data kuchambua na kuandika tasnifu (Kombo na Tromph, 2006)

Usanifu wa utafiti huu ni uchunguzi kifani unaohusu kuteuliwa kwa eneo au jambo maalum ambalo ndilo hushughulikiwa kindakindaki na kupatiwa majibustahiki (Kothari, 2008). Katika utafiti huu wa hadithi za watoto ndiyo iliyoteuliwa kama Uchunguzi wa Dhamira katika hadithi za watoto wilayani Temeke ndiyo zitakazo tafitiwa.

Uchunguzi kifani ni aina nzuri ya usanifu wa utafiti kwa sababu humrahisishia mtafiti shughuli zote za utafiti  kwa sababu tayari ameshajua jambo analoliendea kulitafiti na mwongozo wake utakua kama ifuatavyo.

Utafiti huu utakua wa nyanjani na eneo litakalofanyikia huu ni mkoa wa Dar es salaam katika wilayani Temeke kata ya Kijichi, Mbagala Kuu, Mtoni, Temeke na Chamazi pia maktaba, tovuti mbalimbali zitatumika ili kuongeza maarifa katika utafiti huu.

Mtafiti atazingatia maadili ili kupata matokeo yenye usahihi na ukweli ndani yake hii inamaanisha kabla ya kuanza kutafiti na kukusanya data ni lazima ataomba ruhusa kwa mamlaka yaani katika kata awe na ruhusa ya kuanza kutafiti, atazingatia mavazi kwa kuvaa mavazi yenye heshima na haiba kwa jamii hiyo na utumizi wa lugha fasaha isiyo kuwa na matusi wala kejeli.

Mtafiti ataandaa vifaa vya kufanyia utafiti na atavitunza mahali salama kama vile katika begi au mkoba atakaobeba ili asisahau, ambapo havitapata usumbufu au kuharibika mfano wa vifaa hivyo ni kalamu, karatasi, kamera, simu, penseli, wino wa kufutia na ratiba ya namna atakavyozunguka kutafiti.

Utafiti huu utakua ni shirikishi ili kuleta matokeo bora na mazuri ni lazima kuwe na mashirikiano kwa sababau mada yenyewe ni hadithi inahitaji ushirikiano hivyo mtafiti atashirikisha watoto, walezi, wazazi ambao wanazifahamu vyema hadithi hizo.

Utafiti utakusanya data za aina mbili ambazo ni data za msingi au ghafi zitakuwa ni dhamira ambazo zitapatikana kutoka katika hadithi za watoto wilayani Temeke na za upili hizi zitatumika ili kukamilisha utafiti huu kwa sababu zilishafanyiwa kazi na watafiti wengine mtafiti atapata fursa ya kupitia nyaraka na makala mbalimbali ili kusaidia utafiti huu kwenda mbele zaidi.

Mtafiti atatumia mbinu mchanganyiko za kukusanya data kama vile ushuhudiaji, usaili, dodoso na maktabani ili kukusanya data zenye utimilifu na kuzingatia kanuni za utafiti kwa kufika mapema (yaani muda sahihi pasi na kuchelewa) katika eneo la utafiti ili aende sambamba na ahadi za watafitiwa wake.

Baada ya kukusanya data mtafiti atachambua data kwa kutolea ufafanuzi data zilizokusanywa na hii itakua njia itakayosaidia kujibu maswali ya utafiti ili kutimiza lengo la utafiti hii itafanyika kwa umakini zaidi ili kuepusha kuharibu data zilizokusanywa.

Data za utafiti huu zitachambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo na kwa kuzingatia dhamira katika hadithi za watoto wilayani Temeke.

Mtafiti atatumia mkabala wa kimaelezo hii ni kutokana na uwanja wa kazi hii unahusu lugha hivyo uchambuzi wadata hizi utatumia ufafanuzi wa kimaelezo zaidi ili kufafanua kwa uwazi data ambazo zimekusanywa na kufanyiwa utafiti zaidi.

Mtafiti atachambua data kwa kuzingatia hatua ya kusoma na kuziainisha hadithi hizo, pili kuzichambua dhamiira zitakazotambwa au kutambiwa watoto pamoja na kuchambua ujumbe utakaopatikana katika hadithi hizo.

Data za utafiti huu zitakuwa sahihi kwa sababu zitakusanywa kwa kuzingatia kanuni zote za ukusanyaji wa data katika utafiti kwa kutumia mbinu ya usikilizaji, usomaji na upitiaji makini wa nyaraka na hapo ndipo kutapelekea kuaminika kwa matokeo hayo ya utafiti mara baada ya kupitishwa na msimamizi wa utafiti ndipo mtafiti

ataendelea na hatua nyingine zinazofuata baada ya kupewa ruhusa na msimazizi wa utafiti.

Mtafiti ataandika tasnifu, baada ya kukubaliana na simamizi utafiti kuwa utafiti huo umekizi viwango vinavyohitajika ndipo mtafiti ataandika tasnifu yenye sura tano (hii ni ripoti ambayo huwasilisha matokeo ya uafiti)huwa na suala la utafiti, nadharia tete, malengo, mbinu za utafiti, nadharia iliyotumika, matatizo yalioukumba utafiti, matokeo, mapendekezo, marejeleo na majedwali.

Huu ndio usanifu wa utafiti unavyoonyesha ni jinsi gani utafiti utakavyoanza kufanywa hadi kukamilika.